

KUCHUNGUZA DHIMAZA UTANI WA JADI KATI YA WATU WA  
KIUYU MINUNGWINI NA WA KISIWA CHA KOJANI WILAYA  
YA WETE KASKAZINI PEMBA

BIMIZE HAMAD JUMA

TASNIFU ILIYOWASILISHWA KWA AJILI YA KUTIMIZA SEHEMU YA  
MASHARTI YA KUTUNUKIWA SHAHADA YA UZAMILI YA KISWAHILI  
(M.A KISWAHILI) KATIKA IDARA YA LUGHA NA TAALUMA ZA FASIHI  
YA CHUO KIKUU HURIA CHA TANZANIA

2022

**ITHIBATI YA MSIMAMIZI**

Aliyesaini hapo chini, anathibitisha kwamba, ameisoma tasnifu inayoitwa; *Kuchunguza Dhima za Utani wa Jadi Kati ya Watu wa Kiuyu Minungwini na Kojani Wilaya ya Wete, Mkoa wa Kaskazini Pemba* na anapendekeza ikubaliwe na Chuo Kikuu Huria cha Tanzania, kwa ajili ya kutunukiwa Shahada ya Uzamili katika Idara ya Lugha na Taaluma za Fasihi ya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

.....  
AMOUR RASHID ALI

(Msimamizi)

Tarehe .....

**TAMKO**

Mimi, **Bimize Hamad Juma** nathibitisha kuwa tasnifu hii ni kazi yangu halisi na kwamba haijawahi kuwasilishwa katika Chuo Kikuu kingine chochote, kwa ajili ya masomo ya Uzamili.

**Saini .....**

**Tarehe.....**

**HAKI MILIKI**

Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kuzalisha, kunakili, wala kusambaza sehemu yoyote ya tasnifu hii, kwa namna yoyote, bila ya ruhusa ya mtafiti ama Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

**TABARUKU**

Natabaruku kazi hii kwa mama yangu kipenzi Bi. Tima Nassor Shoka na baba yangu mpendwa Marehemu Bw. Hamad Juma Othman, baba lala salama kaburini uliko, nyinyi ndio mulionilea na kunikuza kielimu hadi leo nimefikia kiwango hiki cha elimu. Aidha, naitabaruku kazi hii kwa mume wangu mpenzi Bw. Ali Vuai Haji. Nawaombea Mwenyezi Mungu awape maisha mema hapa duniani na kesho Akhera. Amin.

## SHUKURANI

Mwanzo kabisa napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu aliyeniumba, kunikuza, kunipa afya, akili na fahamu na nikawa miongoni mwa watembea katika ardhi hii kwa marefu na mapana. Hili ni tunukio kubwa kwangu kwani wapo wale tuliozaliwa siku moja na hata waliozaliwa baadae sasa hawapo tena katika maisha haya ya duniani.

Pili, napenda kumshukuru kwa dhati msimamizi wangu wa utafiti huu MaalimuAmour Rashid Ali ambaye amejaa busara, hekima na ucheshi katika kutoa maelekezo ya kazi hii hadi pale ilipokamilika. Juhudi zake za kipekee sitazisahau maishani mwangu. Naye namuomba Mwenyezi Mungu amfungulie njia ya wepesi kila jambo lake iwe ni sababu ya kuingia peponi baada ya maisha haya mafupi ya kutahiniwa na Mungu.

Tatu, namshukuru mama yangu Bi. Tima Nassor Shoka na baba yangu Hamad Juma Othman kwa kunisaidia na kunitia moyo hadi kukamilika kwa utafiti huu. Aidha, ninawashukuru wanangu wapenzi Sahil Ali Vuai, Yahaya Ali Vuai, Haroun Ali Vuai, Nurdin Ali Vuai, Sabahi Ali Vuai na Sara Ali Vuai kwa uvumilivu wao katika kipindi chote cha masomo yangu. Bila kuwasahau ndugu zangu wote ambao waliniunga mkono kwa kunilelea watoto wangu wakati nikiwa masomoni.

Nne, nawashukuru wahadhiri wangu wote wa Chuo Kikuu Huria cha Tanzania. Hawa ni wengi. Hivyo nitawataja lakini naamini kwamba si hao tu waliosaidia katika ngazi hii ya elimu. Baadhi ya wachache ni Dkt. Mohamed Omary Maguo, Dkt. Hilda Pembe, Dkt. Zelda Elisifa, Mw. Bakar Kombo, Mw. Hemed Said Massoud, Mw. Sharifu Faki na wengineo.

Tano, ninawashukuru kwa dhati wanafunzi wenzangu wote wa fani ya Fasihi ya Kiswahili. Ushirikiano na msaada wao kwangu ulisaidia sana katika kufanikisha masomo yangu. Hapa nawataja kwa uchache, Haji Omar Kombo, Salum Khamis Zubeir, Yussuf Mbwana Ali, Fatma Rashid Ali, Ali Suleiman Shaame, Khamis Hamad Omar, Maimuna Haji Ali, Mahindi Hamad Chum nawashukuru kwa msaada wao mkubwa wa namna ya kuikamilisha kazi hii kivitendo.

Shukurani za pekee nazitoa kwa mlezi wa watoto wangu Bi. Tatu Nassor Chum ambaye alijitolea kuwalea watoto wangu katika kipindi chote cha masomo yangu. Hakika nakiri kwamba bila uvumilivu wake na msaada wake kwangu masomo yangu yangeniwia vigumu. Namuomba Mwenyezi Mungu amlipe kila la kheri na ampe kauli thabiti hapa duniani na kesho Akhera. Amin.

## IKISIRI

Tasnifu hii inahusu Kuchunguza Dhima za Utani wa Jadi Kati ya Watu wa Kiuyu Minungwini na Kojani Wilaya ya Wete, Mkoa wa Kaskazini Pemba. Nadharia iliyoongoza utafiti huu ni nadharia ya Simiotiki na ndharia ya Mwitiko wa Msomaji. Data zilikusanywa kwa kutumia mbinu ya usaili na usomaji makini. Hivyo, matokeo yalikuwa kama ifuatavyo. Lengo mahsusi la kwanza la Utafiti huu lilikuwa ni: Kubainisha aina za utani wa jadi katika jamii ya Kiuyu Minungwini na Kojani. Matokeo ya utafiti huu yalionesha kuwa utani wa jadi wa jamii ya Kiuyu Minungwini na Kojani unaweza kuwekwa katika utani wa misibani, utani wa shuguli za harusi, utani kwenye minada ya bidhaa, utani katika shughuli za uvuvi, utani unaohusu kujitambulisha, utani katika michezo, utani katika kuchumbia wachumba, utani wa matukio ya ajali na huzuni, utani katika vyombo vya usafiri na utani katika shughuli za kilimo. Lengo mahsusi la pili la utafiti huu lilikuwa ni: “Kuchunguza vipengele vya lugha vinavyojitokeza katika utani wa jadi kati ya wanajamii wa Kiuyu Minungwini na Kojani.” Matokeo ya utafiti huu yameonesha kuwa utani wa jadi katika jamii ya Kiuyu Minungwini na Kojani unatumia vipengele vya lugha ambavyo ni lugha ya lahaja, lugha ya kishairi, balagha, dhihaka na lugha ya matusi. Lengo mahsusi la tatu la utafiti huu lilikuwa ni: “Kuchambua dhima za utani wa jadi kwa jamii ya watu wa Kiuyu Minungwini na Kojani.” Matokeo ya utafiti huu yameonesha kuwa utani wa jadi wa jamii ya Kiuyu Minungwini na Kojani una dhima kukuza lugha ya Kiswahili, kuendeleza utamaduni, kukuza fasihi ya Kiswahili, kutambulisha na kuifunza jamii. Dhima nyengine ni pamoja na kukuza umoja na mshikamano, kuhimiza kazi na kuweka hakiba, kuikosoa jamii, kuendeleza mila na desturi za jamii na kuburudisha. Mwisho, utafiti umependekeza kufanyika kwa tafiti zaidi kuhusu fani ya utani na jamii kutumia lugha isiyokuwa na matusi ili kuleta athari chanya ya utani. **Maneno Makuu:** *Utani, Desturi, Simiotiki*



## YALIYOMO

ITHIBATI YA MSIMAMIZI.....	ii
TAMKO.. .....	iii
HAKI MILIKI .....	iv
TABARUKU .....	v
SHUKURANI.....	vi
IKISIRI.. .....	viii
YALIYOMO .....	ix
OROTHA YA MAJEDWALI .....	xiv

### **SURA YA KWANZA: UTANGULIZI.....1**

1.1	Utangulizi.....	1
1.2	Usuli wa Mada.....	1
1.3	Tatizo la Utafiti.....	4
1.4	Malengo ya Utafiti.....	6
1.4.1	Lengo Kuu .....	6
1.4.2	Malengo Mahsusi .....	6
1.5	Maswali ya Utafiti .....	6
1.6	Umuhimu wa Utafiti.....	7
1.7	Mipaka ya Utafiti.....	8
1.8	Mpangilio wa Tasnifu.....	8

### **SURA YA PILI: MAPITIO YA KAZI TANGULIZI NA MKABALA WA**

	<b>KINADHARIA .....</b>	<b>9</b>
2.1	Utangulizi .....	9

2.2	Dhana ya Utani .....	9
1.2.3	Aina za utani.....	11
1.2.3.1	Utani wa Eneo kwa Eneo .....	11
1.2.3.2	Utani wa Binamu.....	11
1.2.3.3	Utani wa Mashemeji.....	12
1.2.3.4	Utani wa Bibi /Babu na Wajukuu.....	12
1.2.3.5	Utani wa Makundi ya Watu.....	13
2.2.2	Lugha katika Kazi ya Fasihi .....	13
2.4	Tafiti za Utani katika Makabila ya Tanzania.....	14
2.5	Tafiti za Utani katika Jamii ya Zanzibar .....	17
2.6	Pengo la Utafiti.....	20
2.7	Nadharia za Utafiti .....	21
2.7.1	Nadharia ya Simiotiki.....	21
2.7.2	Nadharia ya Mwitiko wa Msomaji .....	24
2.8	Hitimisho .....	27
<b>SURA YA TATU: MBINU ZA UTAFITI.....</b>		<b>29</b>
3.1	Utangulizi .....	29
3.2	Usanifu wa Utafiti .....	29
3.3	Eneo la Utafiti.....	29
3.4	Walengwa wa Utafiti.....	30
3.5	Sampuli na Usampulishaji.....	30
3.5.1	Sampuli.....	30
3.5.2	Usampulishaji .....	30

3.6	Ukusanyaji wa Data.....	31
3.6.1	Data za Msingi.....	31
3.6.2	Data za Upili.....	32
3.7	Mbinu za Kukusanya Data .....	32
3.7.1	Mbinu ya Maktabani.....	33
3.7.2	Mbinu ya Usaili .....	33
3.8	Usahihi, Kuaminika na Maadili ya Utafiti .....	34
3.8.1	Usahihi wa Data .....	34
3.8.2	Kuaminika kwa Data za Utafiti .....	34
3.8.3	Maadili ya Utafiti .....	35
3.9	Hitimisho .....	35

## **SURA YA NNE: UWASILISHAJI, UCHAMBUZI NA MJADALA WA**

	<b>DATA ZA UTAFITI.....</b>	<b>36</b>
4.1	Utangulizi .....	36
4.2	Aina za Utani katika Jamii ya Kojani na Kiuyu Minungwini .....	36
4.2.1	Utani wa Misibani .....	36
4.2.2	Utani katika Shughuli za Harusi.....	38
4.2.3	Utani wa Kwenye Minada ya Bidhaa.....	41
4.2.4	Utani wa Shughuli za Uvuvi.....	43
4.2.5	Utani katika Kujitambulisha.....	45
4.2.6	Utani katika Michezo .....	47
4.2.7	Utani katika Kuchumbia.....	48
4.2.8	Utani wa Matukio ya Ajali na Huzuni.....	50

4.2.9	Utani katika Vyombo vya Usafiri.....	51
4.2.10	Utani katika Shughuli za Kilimo .....	53
4.3	Lugha katika Utani wa Kojani na Kiuyu Minungwini .....	54
4.3.1	Matumizi ya Lahaja.....	54
4.3.2	Lugha ya Ushairi .....	56
4.3.3	Balagha .....	57
4.3.4	Kejeli .....	60
4.3.5	Dhahaka.....	62
4.3.6	Lugha ya Matusi .....	64
4.4	Dhima za Utani wa Jadi wa Jamii ya Kojani na Kiuyu Minungwini .....	66
4.4.1	Kukuza Lugha .....	66
4.4.2	Kuendeleza Utamaduni .....	68
4.4.3	Kukuza Fasihi ya Kiswahili.....	70
4.4.4	Kutambulisha.....	72
4.4.6	Kukuza Umoja na Mshikamano .....	74
4.4.7	Kuhimiza Kazi na Kuweka Akiba .....	76
4.4.8	Kuikosa Jamii .....	77
4.4.9	Kuendeleza Mila na Desturi za Jamii .....	79
4.4.10	Kuburudisha .....	81
4.5	Hitimisho .....	82
<b>SURA YA TANO: MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO .....</b>		<b>83</b>
5.1	Utangulizi .....	83
5.2	Muhutasi wa Tasnifu .....	83

5.3	Muhutajari wa Matokeo ya Utafiti.....	85
5.3.1	Lengo Mahususi la Kwanza. Kubainisha aina za utani wa jadi katika jamii ya Kiuyu Minungwini na Kokjani.....	85
5.3.2	Lengo Mahususi la Pili Kuchunguza Vipengele vya Lugha Vinavyojitokeza katika Utani wa Jadi kati ya Wanajamii wa Kiuyu Minungwini na Kojani.....	86
5.3.3	Lengo Mahususi la Tatu Kuchambua Dhima za Utani wa Jadi kwa Jamii ya Watu wa Kiuyu Minungwini na Kojani.....	86
5.4	Hitimisho .....	86
5.5	Mapendekezo.....	87
5.5.1	Mapendekezo kwa Watafiti Wengine .....	87
5.5.2	Mapendekezo kwa Jamii .....	87
	<b>MAREJELEO.....</b>	<b>88</b>
	<b>VIAMBATISHO.....</b>	<b>93</b>

**OROTHA YA MAJEDWALI**

Jedwali la Sampuli ya utafiti ..... 31

## **SURA YA KWANZA**

### **UTANGULIZI**

#### **1.1 `Utangulizi**

Sura hii inashughulikia vipengele vya kiutangulizi vya utafiti huu ambavyo vinahusu usuli wa mada ya utafiti, tatizo la utafiti, madhumuni ya utafiti, maswali ya utafiti huu, umuhimu wa utafiti pamoja na mipaka ya utafiti. Sura hii inabainisha kwa muhtasari kile kilichokusudiwa kutafitiwa.

#### **1.2 Usuli wa Mada**

Kila jamii ulimwenguni ina utamaduni wake ambao hurithiwa kutoka kizazi hadi kizazi. Miongoni mwa tamaduni za jamii mbalimbali ni utani. Utani ni kitanzu cha fasihi simulizi ambacho hutoa fursa kwa watu kuambiana mambo mbalimbali bila kujali kero, chuki na athari zinazoweza kujitokeza. Senyamanza (2012) anaeleza kwamba utani ni uhusiano wa kijamii unaoruhusu watu kufanyiana dhihaka na kejeli. Kimuundo utani huweza kuwa katika umbo lanyimbo, matendo au hadithi fupi fupi. Anaendelea kueleza kuwa utani ni kipengele maarufu sana katika jamii nyingi za hapa Tanzania na Afrika kwa ujumla wake. Umaarufu na kuzoeleka kwake kumesababisha uonekane kama ni kipengele cha lazima katika maisha ya kila siku. Kuhusu umuhimu wa utani katika jamii, Mulokozi (1986) na Ponera (2010) wana mawazo yanayofanana na maelezo haya na kusema kwamba suala la utani ni jadi ya Waafrika ambayo ina taratibu na kaida mbalimbali.

Hata hivyo, Sengo (1975) anapingana na maelezo yaliyoelezwa hapo juu pale anapodai kwamba utani uliletwa Tanzania na wafanyabiashara wa Kiarabu, na hatimaye ukaignwa na kuingizwa katika mikondo ya taratibu na mwenendo wa

maisha ya mwanadamu. Mawazo haya yanawiyana na yale ya Sikazwe (1974), Kyando (1973) na Mahundi (1971) ambao wanaeleza kuwa chanzo kikuu cha utani katika makabila mengi ni biashara na vita. Wanatolea mifano katika kabila la Wangoni na Wanyamwezi, Wakinga na Wasafwa. Utani wao umekuwa kutokana na mahusiano ya kibiashara. Wahehe na Wakinga, Wavidunda na Wangoni, utani waoumetokana na vita.

Kwa maoni ya mtafiti ni kwamba mawazo ya Sengo (1975), Sikazwe (1974), Kyando (1973) na Mahundi (1971) yana mapungufu na yanahitaji kufanyiwa uchunguzi ili kubaini ukweli wa suala hili. Hii ni kwasababu, utani katika jamii upo katika nyanja mbalimbali za maisha kama vile kazi, harusi, misiba, mahusiano nakadhalika. Kwa sababu hii Watanzania hawakusubiri hadi majilio ya Waarabu ndio wakaanza kuwa na utanzu wa utani kama anavyoeleza Sengo.

Hadi sasa hakuna mgawanyo wa moja kwa moja unaobainisha aina za utani zinazopatika katika jamii, bali aina za utani hutegemea namna jamii inavyoendeleza utani katika vipengele anwaai. Hata hivyo, wataalamu wamekuwa wakibainisha aina za utani kwa mwelekeo unaofanana. Mathalani Senyamanza (2012) anaeleza kuwa jamii nyingi za Tanzania utani hujidhihirisha katika aina nne ambazo ni kati ya kabila na kabila, mjomba nawapwawe, mashemeji pamoja na utani baina ya babu au bibi na wajukuu. Naye, Mlaga (2017) anaainisha aina kama hizo kwa kusema kwamba utani huweza kujidhihirisha kwa kutegemea uhusiano wa wahusika ambapo anapata aina tano za utani ambazo ni utani wa mabibi/mababu na wajukuu, utani wa mashemeji, utani wa kikabila, utani wa marafiki kama vile Yanga na Simba na utani wa watu wanaoamua kushindana na kutaniana mbele ya hadhira.



Kila fasihi ina dhima katika jamii. Hivyo, Mgunda (2014) anaeleza kwamba utani kama kipengele kimojawapo cha fasihi simulizi una dhima ya kudumisha na kuendeleza fasihi kwa madhumuni ya kukuza mahusiano ya kijamii, kutatua migogoro, kuimarisha mashirikiano katika jamii. Pia, utani hukuza maadili kwa kutoa mafunzo na malezi kuhusiana na maisha, mila nadesturi za jamii. Naye Sengo (1975) ana mawazo yanayolingana na hayopale anapoeleza kuwa wale wanaoufahamu utani hutumia kama chombo cha maadili katika maisha na udugu usio mfano. Yote hayo huelezwa kwa kutumia lugha ya kisanii. Mgunda (ktj), anaeleza kuwa wanajamii wamekuwa wakitumia maneno makali yenye mafumbo, vijembe na kejeli na wakati mwingine hutumia nyimbo katika kukuza na kudumisha utani.

Miaka ya hivi karibuni, tafiti kadhaa kuhusu utani zimekuwa zikifanywa ingawa bado ni chache. Kama wasemavyo Lucas na Sengo (1975) kwambakatika jamii za Waswahili tafiti zihusuzo utani zilichelewa kufanywa kwani utani haukuonekana kuwa jambo la msingi na lenye faida. Lakini kwa sasa tafiti zinazohusu utanizimefanywa na baadhi ya wataalamu mbalimbali ingawa zinatofautiana kwa kiasi kwani kila mtaalamu ana maswali na malengo ya utafiti wake.

Miongoni mwa wale waliowahi kufanya utafiti unaohusu utani ni Radcliffe-Brown (1940) ambaye alifanya uchunguzi katika jamii za Afrika Mashariki na kugundua kwamba utani ni uhusiano wa kufanyiana masihara ambao ni tofauti na desturi ya kutokuheshimiana. Madhumuni yake makubwa ni kupunguza na kuondoa kabisa uhasama na chuki iliopo baina ya udugu huo.

Nao Lucas na Sengo (1975) walichunguza utani katika jamii ya Wakerewe. Katika utafiti huo waligundua kuwa utani ni chuo cha kutunza maadili ya jamii ya Wakerewe. Vile vile, Gora (2015) alifanya utafiti katika jamii ya Watumbatu akiwa na mada isemayo “Utani katika Sherehe za Harusi za Watumbatu: Aina, Sababu na Taathira”. Katika utafiti huo aligundua kuwa Watumbatu wamekuwa wakifanyiana utani unaojikita kati ya babu au bibi na wajukuu, utani wa mashemeji, utani wa marafiki na utani wa watu wanaoamua kushindana na kutaniana mbele ya hadhira.

Jamii za Kiuyu Minungwini na Kojani zimekuwa na utani wa jadi kwa miongo kadhaa. Mtafiti alifanya mazungumzo na Mzee Ali Issa Ali wa Kojani na Mzee Saidi Makame Hamad wa Kiuyu Minungwini na kueleza kuwa jamii hizo hapo kabla zilikuwa moja kwa sababu watu wa Kiuyu Minungwini wanatoka katika jamii ya Wakojani. Wanaendelea kueleza kuwa jamii hizo zimekuwa na historia ndefu katika kufanyiana utani katika shughuli za harusi, misiba, matanga, kazi, viwanja vya michezo, ndoa, shughuli za uvuvi, kilimo nakadhalika. Utani huo hutoa fursa kwa wanajamii kuelezana mambo kadhaa bila ya uficho ingawa lugha inayotumika mara nyengine siyo ya moja kwa moja. Hata hivyo, pamoja na jamii hizo kutumia utanzu huu katika maisha yao ya kila siku hadi sasa mtafiti hajaona utafiti uliowahi kufanyika ukiwa na lengo la kuchunguza dhima na matumizi ya lugha katika utani wa jadi wa jamii hizo. Hivyo mtafiti aliona ipo nafasi ya kufanya utafiti huu.

### **1.3 Tatizo la Utafiti**

Utani ni utamaduni uliozoeleka sana katika jamii nyingi za Afrika. Watu hutaniana katika shughuli kama vile harusi, matanga, michezo, kazi nakadhalika. Wapo watafiti kadhaa ambao wamewahi kujishughulisha na fasihi ya utani. Miongoni mwa

hao ni, Red Cliffe Brown (1940), Mahundi (1971), Kyando (1973), Sikazwe (1974), Sengo (1975), Senyamnza (2012), Mgunda (2014), Gora (2015) na Mlaga (2017). Mathalini Gora (2015), alifanya uchunguzi ambao ulijikita kuchunguza namna utani unavyofanyika katika sherehe za harusi katika jamii ya Watumabatu. Katika utafiti huo Gora (keshatajwa) aligundua kwamba kuna aina nne za utani ufanyikao katika sherehe za Watumbatu. Amezitaja aina hizo kuwa ni utani wa binamu, utani wa mashemeji, utani wa babu/ bibi na wajukuu na utani wa marafiki. Utani katika jamii hii hufanywa kwa sababu ya kujitambulisha, kuonesha mahusiano, kufunza na kuburudisha. Aghalabu, utani katika jamii ya Watumbatu katika sherehe za harusi hutawaliwa na matumizi ya matusi na kejeli ambazo huwa na taashira maalumu iliyokusudiwa. Sengo na Lucas (1975), kwa upande waowamefikia hitimisho kuwa chanzo cha utani ni shida au matatizo kama vile njaa, vita na mafuriko mengine makubwa. Sengo na Lucas (weshatajwa) wameugawa utani katika, daraja za kifamilia, kijirani, kibinamu, kikabila na kadhalika. Rashid (2011) alifanya utafiti kuhusu namna utani unavyotumika kisiwani Pemba. Katika utafiti wake alibaini kwamba, utani unachukua nafasi kubwa katika maeneo ya kazini kama vile kwenye ukuli, ukwezi na uvuvi. Pia, umefanyiwa utafiti kwa kuuhusisha zaidi na makabila ya Tanzania Bara. Pamoja na juhudi zilizowahi kufanyika za kutafiti za utani. Utalii uliofanywa na mtafiti umebaini kwamba utafiti kuhusu utani umefanywa kwa kiasi kidogo katika jamii ya Zanzibar. Uhalisia huo ulichochea hamu ya mtafiti kutaka kufanya utafiti katika jamii ya Kojani na Kiuyu Minungwini. Katika jamii hizi mbili utani umekuwa ni sehemu ya utamaduni wao. Hivyo tatizo la utafiti huu ni kutaka kubainini kwa namna gani utani wa jadi wa jamii ya Kojani na Kiuyu

Minungwini unavyobeba dhima mbalimbali kwa wanajamii na namna unavyotumia vipengele vya lugha, ili kupunguza mwanya ulioachwa na watangulizi wake.

#### **1.4 Malengo ya Utafiti**

Utafiti huu una lengo kuu na malengo mahsusi yafuatayo:

##### **1.4.1 Lengo Kuu**

Lengo kuu ni Kuchunguza dhima za utani wa jadi na namna fani hiyo inavyotumia lugha katika jamii ya watu wa Kiuyu Minungwini na Kojani.

##### **1.4.2 Malengo Mahsusi**

Malengo mahsusi ni:

- i) Kubainisha aina za utani wa jadi katika jamii ya Kiuyu Minungwini na Kojani
- (ii) Kuchunguza vipengele vya lugha vinavyojitokeza katika utani wa jadi kati ya wanajamii wa Kiuyu Minungwini na Kojani.
- (iii) Kuchambua dhimaza utani wa jadi kwa jamii ya watu wa Kiuyu Minungwini na Kojani.

#### **1.5 Maswali ya Utafiti**

Utafiti huu umeongozwa na maswali ya utafiti yafuatayo:

- (i) Ni aina zipi za utani wa jadi zinazojitokeza katika jamii za Kiuyu Minungwini na Kojani?
- (ii) Ni vipengele vipi vya lugha vinavyojitokeza katika utani wa jadi kati ya wanajamii wa Kiuyu Minungwini na Kojani?

(iii) Ni dhima zipi zinazojitokeza katika utani wa jadi wa wanajamii wa Kiuyu Minungwini na Kisiwa cha Kojani?

## 1.6 Umuhimu wa Utafiti

Utafiti huu utakuwa na umuhimu kama ifuatavyo:

**Kitaaluma:** Matokeo ya utafiti huu yatakuwa marejeleo kwa wasomi wa ngazi zote za taaluma ya fasihi. Wanafunzi, walimu na wasomi wengine wa kazi za fasihi wanategemewakuyatumia matokeo ya utafiti huu kama sehemu ya marejeleo yao ya kukamilisha malengo na madhumuni ya utafiti watakaokuwa wanaufanya. Aidha, matokeo ya utafiti huu yanategemewa kutumika kama sehemu ya kujiimarisha, ili kubainisha pengo la utafiti ambalo wao watalishughulikia katika tafiti zao. Wanataaluma ambao ni walimu na wahadhiri katika taaluma ya fasihi watauona umuhimu wa utafiti huu katika kuandika vitabu, makala na maandalio ya masomo ya kufundishia wanafunzi wa ngazi tofauti za elimu hasa katika uwanja unaohusu fasihi ya utani.

**Kinadharia:** Utafiti huu unatoa uthibitisho kwamba, nadharia za uhakiki wa fasihi zinapotumika kuhakiki kazi za fasihi huifanya kazi hiyo kuwa imara na yenye mashiko ambayo huaminika kitaaluma. Kupitia utafiti huu watafiti wa baadaye watapata mwongozo wa kuzitumia nadharia ya Simiotiki na Mwitiko wa Msomaji katika kazi zao. Hii ni kwa sababu nadharia hizi zimejidhihirisha katika kazi hii kivitendo, jambo ambalo linatoa mwongozo katika uchambuzi wa kazi za fasihi hasa katika uwanja wa kutathmini dhima na matumizi ya vipengele vya lugha.

**Kijamii:** Utafiti huu unaonesha namna utani unavyoweza kutumika kama nyenzo muhimu ya kijamii ambayo imekusanya dhima mbalimbali ambazo zinatija kwa

jamii husika. Hivyo basi, kwa kutumia utafiti huu jamii inachochewa kutumia utani kwa misingi iliyobora zaidi ili kuendeleza uhusiano ulio bora.

### **1.7 Mipaka ya Utafiti**

Kama ilivyoelezwa hapo kabla kwamba kila jamii inatumia utani katika kila kipengele cha maisha yao. Kwa sababu hiyo, haikuwa rahisi kutafiti utani wa kila jamii kwa wakati mmoja. Hivyo katika utafiti huu mtafiti alijikita kutafiti dhima na matumizi ya lugha katika utani wa jadi wa jamii ya Kiuyu Minungwini na Kojani. Utani unaotokea kwenye vijiji vyengine kisiwani Pemba haukuhusishwa katika utafiti huo.

### **1.8 Mpangilio wa Tasnifu**

Tasnifu hii ina sura tano. Sura ya kwanza imebainisha vipengele vya utangulizi ambavyo ni vya msingi katika utafiti wowote wa kitaaluma. Vipengele hivyo ni pamoja na usuli wa mada, tatizo la utafiti, malengo ya utafiti, maswali ya utafiti, umuhimu wa utafiti, mipaka ya utafiti na muundo wa tasnifu. Sura ya pili inahusu mapitio ya kazi tangulizi na mkabala wa nadharia zilizoongoza utafiti huu na sura ya tatu inabainisha mbinu za utafiti. Sura ya nne ni uwasilishaji na uchambuzi wa data za utafiti na sura ya tano ni ya mwisho katika utafiti huu. Sura hii imetoa muhtasari, hitimisho na mapendekezo ya utafiti.

## **SURA YA PILI**

### **MAPITIO YA KAZI TANGULIZI NA MKABALA WA KINADHARIA**

#### **2.1 Utangulizi**

Hii ni sura iliyowasilisha mapitio ya kazi tangulizi na mkabala wa nadharia. Vipengele muhimu vilivyofafanuliwa kwenye eneo hili ni dhana ya utani, dhima za kazi ya fasihi, jadi na mapitio ya tafiti kuhusu utani. Mapitio hayo yamemuwezesha mtafiti kubainisha pengo la utafiti lililotafitiwa. Mwisho sura hii imefanya ufafanuzi wa nadharia ya Simiotiki na nadharia ya Mwitiko wa Msomaji ambazo zimeongoza uchambuzi wa utafiti huu na mwisho sura hii imetoa hitimisho.

#### **2.2 Dhana ya Utani**

Wamitila (2003) anaeleza kuwa utani ni dhana inayotumiwa kueleza hali ya kufanyiana mzaha miongoni mwa wanajamii au jamii mbalimbali bila kuogopa au kushitakiana. *Kamusi ya Kiswahili Sanifu* (2010) inafafanua kuwa dhana ya utani kuwa ni maneno au vitendo vya dhihaka au mzaha. Watu hufanyiana mzaha kwa lengo la kuambizana ukweli na kuimarisha mahusiano.

Baadhi ya watu huona kuwa utani ni tendo la kufanyiana masihara. Hata hivyo, mawazo hayo yanamapungufu tunapoelezea utani katika jamii. Kwani kwa mujibu wa Kyando (1993) utani ni zaidi ya masihara Kyando (keshatajwa) anazidi kufafanua kwa kusema kwamba, masihara ni sura ndogo tu ya utani. Anendelea kueleza kuwautani ni mahusiano yanayojengeka katika jamii yenye lengo la kukuza ushirikiano na mahusiano katika jamii. Naye Senyamanza (2012) anaufafanua utani kuwa nikamakipengele cha lazima katika jamii. Hoja hii kwa kiasi ni ya kweli kwa

sababu jamii nyingi za hapa Tanzania na Afrika kwa ujumla zimeufanya utani kuwa ni jambo la lazima katika maisha yao ya kila siku.

Mtaalamu mwingine aliyewahi kuzungumzia utani ni Mulokozi (1999) ambaye alieleza kuwa suala la utani limeenea sana katika jamii ya Buhaya na katika jamii nyingi za Kiafrika. Suala hili kikawaida hutawaliwa na taratibu na kaida mbalimbali za kijamii. Utani si neno geni katika maisha ya mwanadamu wengi wetu twaona ni maneno au vitendo vya dhihaka, kejeli au mzaha bila kujua asili ya neno lenyewe.

Nguro (2005) anasisitiza kuwa, utani ni fani ya kipekee katikafasihi simulizi na ina sura kubwa katika maisha ya kila siku. Aghlabu, utani hufanywa kwa njia ya malumbano, mtu mmoja anamtania mwingine na kujibiwa hapo hapo, watu hutania harusini, ngomani, katika hadhara za pombe na matangani. Maelezo haya yanayakinisha kuwa utani ni kipengele muhimu katika maisha ya kila siku.

Ngure (2003) na Mulokozi (1996) wanaainisha utani kwa mawazo yanayokaribiana ambapo wanauainisha katika mafungu matano ambayo ni utani kati ya ukoo na ukoo, utani kati ya ndugu na ndugu, utani kati ya kabila na kabila, utani kati ya rafiki na marafiki na utani kati ya watu wa mkoa na mkoa. Mawazo hayo yameongoza tasnifu hii na imebaini kuwa utani unaweza kufanywa na jamii zaidi ya moja na si tu kabila moja kutania kabila jengine.

Mawazo ya wataalamu hawa yamempatia uelewa mtafiti kuwa utani ni fani ya fasihi simulizi ambayo fanani hupata fursa ya kutania na hadhira kwa kutumia lugha ya dhihaka, kejeli, mafumbo nakadhalika. Kwa kutumia utani wahusika hupata fursa ya kujitambulisha, kukosoa, kufundisha, kufurahisha nakadhalika. Mara nyengine lugha



inayotumika huwa imejaa matusi na dhihaka hata hivyo, si kawaida lugha hiyo kuibua mtafaruku miongoni mwa hadhira.

### **1.2.3 Aina za utani**

Utani umekuwa ukibainishwa kwa vigezo tofauti tofauti. Kutokana na hali hiyo hakuna mgawanyo uliorasmi katika ubainishaji wa utani miongoni mwa wanafasihi. Pamoja na ukweli huo watafiti kama vile Sengo na Lucas (1975), Mulokozi (1996), Simiyu (2011) na Othman (2015) wamebainisha utani katika matapo yafuatayo:

#### **1.2.3.1 Utani wa Eneo kwa Eneo**

Aina hii ya utani huhusisha makundi ya watu ambao huishi katika eneo moja na jengine. Kigezo kikuu cha kubainisha utani wa aina hii ni kigezo cha kijografia. Utani wa aina hii hujikita kupandisha hadhi ya eneo moja na kudharau eneo jengine. Mfano wa utani wa kimaeneo ni utani unaopatikana kati ya jamii ya Kojani na jamii ya Kiuyu Minungwini ambazo zilikuwa ni kiini cha utafiti huu. Jamii hizo zimekuwa zikitania kwa kujikuza na kudogesha wengine katika tabia, sifa na matendo.

#### **1.2.3.2 Utani wa Binamu**

Aina hii ya utani hujumuisha watu wanaotokana na ukoo mmoja. Othman (2015) anaeleza kuwa wahusika wakuu wa aina hii ya utani ni watoto waliozaliwa na mjomba au shangazi na watoto waliozaliwa na mama mdogo au mama mkubwa. Uhusiano wa kiutani kwa watu hawa huwa wa maneno na matendo. Kwa mfano mtoto wa kiume wa mjomba anapofunga ndoa nje ya ukoo wao anaweza kuambiwa ameowa mke mbaya hata kama ni mzuri. Hilo hufanyika kama ada ya kumpokea shemeji yao. Kwa kulifahamu hilo hata Bi. Harusi anayetaniwa huwa hachukii kwa

kuambiwa hivyo, kwa vile anajua kuwa huo ni utani miongoni mwa ndugu wa familia. Mara nyengine lengo la utani huo hufanyika ili kujitambulisha.

### **1.2.3.3 Utani wa Mashemeji**

Kwa mujibu wa BAKIZA (2010) neno shemeji ni lakabu anayotumia mwanamume kumwita mke au mume wa ndugu yake. Visawe vya shemeji ni mramu au muwamu. Kundi hili hutuibulia utani unaoweza kubainishwa kama utani wa mashemeji. Kutokana na uhusiano huo, kundi hilo hutaniana na mara nyengine kufikia mtu kuweza kumwita mke wa kaka yake kuwa mkewe au ndugu wa mume wake kuwa mume. Katika jamii za Uswahilini, wanawake wanapofunga ndoa wanatahadharishwa kuwa makini kuhusu utani wa mashemeji kwa sababu baadhi ya utani wa mashemeji unaweza kuharibu ndoa yake, wasije wakatoka katika mila na desturi za jamii zao.

### **1.2.3.4 Utani wa Bibi /Babu na Wajukuu**

Hii ni aina ya utani ambao babu au bibi huwatania wajukuu wake. Kila mwanajamii hujikuta akitumia utani wa aina hii, kutokana na ukweli kwamba kila mwanajamii ana babu au bibi na hata wajukuu. Othman (2015), anawanukuu Ogacho (1974) na Chogero (1975) ambao wanaeleza kuwa wajukuu wanaweza kuwa huru kuuliza maswali na kujifunza mambo mbalimbali ya kimaisha ikiwemo uwajibikaji katika kazi, dawa za asili, utunzaji wa familia na masuala ya ndoa. Uhusiano wao wa kiutani huwa endelevu hata baada ya bibi au babu kufariki. Wakati wa msiba wa marehemu wajukuu wanaweza kufanya utani kwa wazee wao, na hawatulii mpaka wazee watoe pesa ndio salama ipatikane. Mulokozi (1996) anaeleza namna babu

anavyomtania mjukuu wake mara baada ya kuzaliwa. Hii ni kusema kuwa uhusiano wa utani huu huanza tangu mtoto haelewi chochote.

Kwa muhtasari mtafiti ameweza kupata uelewa kuhusu namna ya kubainisha aina za utani uliomo katika jamii. Mawazo yaliyoelezwa katika sehemu hii yalomwezeshamtafiti kubainisha data za utafiti zinazohusu ubainishaji wa aina za utani unaojitokeza katika jamii ya Kiuyu Minungwini na Kojani.

#### **1.2.3.5 Utani wa Makundi ya Watu**

Aina hii ya utani huibuka kutokana na shughuli za kijamii na kiuchumi. Shughuli hizo ni kama vile harakati za maofisini, sokoni, bandarini, mashulenikatika maeneo yanayoendeshwa minada ya kuuza na kununua, harusini nakadhalika. Aina hii ya utani huibuka kutokana na uhusiano wa shughuli katika miktadha husika. Kwa mfano, iwapo muktadha uliopo ni katika michezo kama vile mpira wa miguu, utani utakuwa umejikita katika michezo, vivyo hivyo iwapo muktadha wa sherehe ya harusi utani utakaoibuka ni utani unaohusu shughuliza harusini.

#### **2.2.2 Lugha katika Kazi ya Fasihi**

Lugha ya kisanaa katika fasihi ndio uti wa mgongo wa kazi ya fasihi. Bila kuwa na sanaa ya lugha ni mwiko kuwa na fasihi. Mawazo haya yanaenda sambamba nayale yaliyowahi kusemwa na Ndungo na Mwai (1991) ambao wanaeleza kwamba lugha katika fasihi ni kipengele muhimu sana kwani huitofautisha fasihi na sanaa nyingine yoyote ile. Usanii wa mtunzi wa kazi ya fasihi hutegemea jinsi alivyochagua maneno na kuyatumia kwa njia ya mantiki katika kazi yake. Mtunzi bingwa ni yule aliyeifinyanga lugha na kuliwasilisha lengo lake kwa njia ya mvuto wa hadhira yake.

Hii ni kusema kwamba watunzi wa kazi za fasihi hutofautiana katika matumizi ya lugha ya kisanaa.

Naye Khatibu (1986) anaeleza kuwa katika kazi za fasihi ikiwemo fasihi ya Kiswahili lugha ya sanaa ndio msingi wa kufinyanga fasihi hiyo. Tangu zote za fasihi kama vile shairi, tenzi na nyimbo hutumia vipengele vya lugha katika kusawiri maisha ya jamii. Vipengele hivyo vya lugha kama vile semi vimeshehenezwa usanii ili viweze kuteka masikizi na maoni ya hadhira.

Hivyo katika utafiti huu mtafiti alichunguza vipengele vya lugha namna vinavyotumika katika utani wa jadi wa jamii ya Kiuyu Minungwini na Kojani. Kwa ujumla, imebainika kuwa utani ni kitanzu cha fasihi ya masimulizi ambacho kimekuwa kikitumia matumizi ya aina kwa aina. Msingi mkubwa wa matumizi ya lugha katika fani hii hulenga kuonesha kejeli na dhihaka ili kukosoa, kujitambulisha, kuelimisha nakadhalika.

#### **2.4 Tafiti za Utani katika Makabila ya Tanzania**

Tafiti kadhaa zimewahi kufanyika katika makabila mbali mbali hapa Tanzania. Mathalani, Sengo na Lucas (1975) walifanya utafiti wenye mada inayohusu “Utani wa Jamii ya Ukwere”. Katika utafiti huo, Sengo na Lucas (weshatajwa) wanaeleza kuwa chimbuko la utani katika jamii ya Wakwere ni kutokana na hali za kijamii kama vile shida, njaa, vita, na matokeo makubwa yeyote yaliyowahi kuikumba jamii hiyo. Katika kubainisha aina za utani, Sengo na Lucas wanasema kuwa upo utani wa kifamilia, kijirani, kibinaamu na kikabila. Aidha, katika utafiti huo, wanaeleza kwamba lugha inayotumiwa na watani huwa teule na inayokubalika kutegemea muktadha husika. Lugha hiyo hutumika kufurahisha hadhira pamoja na kuwafanya

wasikilizaji watafakari. Utafiti wa Sengo na Lucas (washatajwa) ingawa ulifanyika katika jamii tofauti na jamii iliyotafitiwa katika utafiti huu, lakini ulisaidia kufikia malengo ya utafiti kutokana na kuonesha namna utani unavyotumia vipengele vya lugha na namna unavyotumika miongoni mwa makundi mbalimbali ya kijamii. Kwa sababu hiyo mtafiti alipata uelewa wa namna ya kubainisha aina za utani na namna ya kufanya uchambuzi wa matumizi ya lugha yanayotokana na fani ya utani.

Utafiti mwengine uliojikita kuchunguza utani ni ule uliofanywa na Waziri na Dlouline (1998) ambao walichunguza jinsi utani ulivyochangia amani na utengamano katika jamii ya Wapare iliyoko Kaskazini mwa Tanzania. Katika utafiti huo, vita vya kikabila miongoni mwa Wapare vinaelezwa kuwa ndio chimbuko la utani wa jamii hiyo. Utafiti wa Waziri na Dlouline (keshatajwa) ulikuwa na manufaa makubwa katika kufikia malengo ya utafiti huu kutokana na kwamba utani katika jamii hiyo ulichunguza namna unavyoakisi dhima mbalimbali kwa jamii kama ilivyofanyika katika utafiti wa utani wa jamii ya Kiuyu Minungwini na Kojani. Tofauti kati ya tafiti hizi ni eneo la kijografia ambapo utafiti ulifanyika.

Nao, Suta na Mnyamba (1999) walifanya uchunguzi wakiwa na lengo la kuchunguza namna utani ulivyochangia katika kuhuisha amani na utengamano miongoni mwa wanajamii wa Bena nchini Tanzania. Matokeo ya uchunguzi huo yalionesha kuwa utani katika jamii ya Wabena umekuwa na dhima ya kuimarisha uhusiano mwema miongoni mwa wanajamii wa Bena. Aidha, utani umekuwa na dhima ya kuimarisha uhusiano mwema miongoni mwa wanajamii, hutumika kutatua migogoro yao, kufunza na kurithisha maadili mema na kuonesha nafasi ya vijana katika jamii. Utafiti huu kama zilivyokuwa tafiti nyingine zilizoelezwa ulikuwa na umuhimu

mkubwa katika kufikia lengo la utafi. Hii ni kwa sababu utafiti huu ulishughulikia dhima za utani kama ilivyofanyoika katika utafiti huu. Hivyo utafiti huo ulikuwa kielelezo cha namna ya kuzibainisha dhima za utani katika jamii ya Kiuyu Minungwini na Kojani.

Vile vile, Mgakazi (2010) alifanya uchambuzi unaohusu namna utani wajamii ya Wasukuma unavyotendeka. Katika ufafanuzi wake Mgakazi (keshatajwa) anaeleza kuwa utani wa jamii hiyo umekuwa ukitendeka kwa kutumia usimulizi, nyimbo, matendo, furaha na hadithi ndefu. Aidha, anaonesha maeneo ambapo utani unaweza kufanyika. Kwa ujumla katika jamii hiyo, utani hujikita zaidi katika sherehe. Watani huwa wanafanya utani mbele ya hadhira hadi pale watakapopewa pesa. Ikitokea hawakupewa pesa huamua kufanya fujo. Utafiti huu ulimsaidia mtafiti kupata dhana ya utani na namna unavyoweza kutendeka katika jamii iliyotafitiwa. Hivyo mtafiti alichunguza namna muktadha wa sherehe kama vile harusi unavyoibua utani ndani yake.

Mwisho, Mzandi (2011) ametafiti mahusiano ya kibiashara katika utani kati ya Wahehe na Wangoni. Katika utafiti huo alichunguza namna ucheshi unavyoibuliwa wakati wa kuuza na kununua. Maelezo haya yanaonesha kwa kiasi gani mahusiano miongoni mwa wanajamii yanavyoweza kuzalisha utani. Mawazo hayo pia yalikuwa ni ya msingi katika utafiti huu. Hii ni kutokana na kwamba ingawa mahusiano sio jambo pekee linaloibua utani katika jamii iliyotafitiwa, kwa kiwango kikubwa uhusiano miongoni mwa wahusika ndio kulikomuwzesha mtafiti kubainisha aina za utani kama zilivyobainishwa katika sura ya nne ya utafiti huu.

## **2.5 Tafiti za Utani katika Jamii ya Zanzibar**

Zanzibar ni sehemu ya Jamuhuri ya Mungano wa Tanzania. Jamii hiyo kama zilivyo jamii za Tanzania Bara nayo imekuwa ikitumia utani katika maeneo mbalimbali. Pamoja na kwamba hadi sasa bado kuna tafiti chache zilizowahi kushughulikia utani katika jamii hiyo ya Zanzibar, juhudi za watafiti zimekuwa zikifanyika ili kufanya uchunguzi wa utanzu huo katika visiwa hivyo. Miongoni mwa watafiti waliochunguza utani katika visiwa hivyo ni Iddi (2005) ambaye alifanya uchunguzi ukiwa na mada “Utani katika Jamii ya Wazanzibari.” Katika utafiti huo alichunguza utani unaojitokeza katika nyimbo za harusini. Anaeleza kuwa katika sherehe ya harusi, maharusi hufanyiwa singo lenye kuambatana na nyimbo za utani ambazo huwa na lengo la kufundisha maharusi hao. Utafiti wa Iddi(keshatajwa) ulikuwa na umuhimu katika kufikia lengo la utafiti huu. Kwanza ulimuwezesha mtafiti kubaini namna utani unavyoweza kujidhihirisha katika kipera cha nyimbo. Pili, utafiti huo umemuwezesha mtafiti kubaini namna mafunzo ya utani yanavyoweza kujidhihirisha katika utani wa sherehe za harusi ambapo ni moja ya aina ya utani unaopatikana katika jamii ya Kiuyu Minungwini na Kojani.

Khamis (2008) aliandika makala yenye anuani “Utamaduni wa Mzanzibari.” Katika makala hiyo anaeleza kuwa Wazanzibari wana desturi ya kufanyiana utani. Miongoni mwa utani wa Wazanzibar ni pamoja na kuitana majina ya utani ambayo huwa maarufu hadi kufikia jina lake la mwanzo kusahaulika. Aidha, wanaeleza kuwa jamii ya Wazanzibar wanamazoea ya kufanyiana utani wakati wa harusi. Watani wa uzawa wa mwanamke anaeolewa humkimbiza harusi asiolewe au mume asioe. Wengine huukamata mkono wa muozeshaji na kudai aozeshwe yeye. Wafungaji wa

mlango ama yule aliyekamata mlango hufanya hivyo mpaka apewe pesa kidogo na ndipo aondoke na kuacha shughuli iendelee. Madhumuni ya kufanya hivyo ni kujitambulisha kuwa yeye ni shemegi yake au mtu wa karibu katika familia. Hapa tunapata taswira kuwa jamii ya Wazanzibari inaikubali jadi hii ya utani katika sehemu mbalimbali. Makala hiyo ya Khamisi pia ilikuwa na mchango mkubwa katika utafiti huu kutokana na kubainisha namna utani wa Wazanzibar unavyojidhihirisha wakati wa harusi. Hivyo mtafiti alichukua mawazo hayo ili kubaini namna dhima zinazodokezwa na Khamisi zinavyojitokeza au zisivyojitokeza katika utani wa jamii ya Kiuyu Minungwini na Kojani.

Uchunguzi mwingine uliowahi kujikita kuchunguza utani ni ule wa Rashid (2010) ambao ulijikita kuchunguza athari za lugha ya utani kwa jamii ya Wapemba. Katika utafiti huo aligundua kuwa utani unahusisha taratibu ambazo zimekubaliwa na jamii husika ambazo wanajamii huambatana maneno na kutendeanana vitendo vinavyokubalika na jamii hiyo. Iwapo ni dhihaka au masihara huwa hakuna chuki inayoweza kuibuka kutokana na maneno hayo. Mawazo haya yalimsaidia mtafiti kubainisha vipengele vya lugha hasa vinavyohusu kejeli na dhihaka kama vinavyojitokeza katika utani wa jamii ya Kiuyu Minungwini na Kojani.

Naye Zeid (2011) alifanya utafiti unaohusu “Athari ya Lugha ya Utani kwa Jamii ya Wapemba”. Katika utafiti huo mtafiti ameeleza kuwa katika kisiwa cha Pemba bado utani una nafasi muhimu katika maisha ya kila siku. Kwa vile utani umetawala katika sehemu za jamii, haifikiriwi kama kuna mtu kwa njia moja au nyengine asiyeshiriki katika harakati za utani katika jamii ya Wapemba, na kufahamisha kuwa utani hufanywa katika miktadha ya mazishini, matangani, harusini na katika



shughuli za kiuchumi. Pia, mtafiti anaeleza kwamba utani umetawaliwa na semi zenye kuashiria kejeli, dhihaka, matusi, na dharau. Semi hizo hujitokeza na kupotea na hakuna semi inayotumika daima. Mtafiti amezungumzia utani kwa jamii ya Wapemba lakini aliegemea katika fani ya isimu na alitazama zaidi athari ya vitendo neni katika lugha ya utani. Kazi hii ilikuwa na tija kubwa katika kufikia malengo ya utafiti uliofanyika. Kwanza, kwa kutumia utafiti huo mtafiti aliweza kubainishaaina za utani kama unavyojitokeza katika jamii teule. Pia, utafiti huo ulionesha namna matumizi ya lugha yanavyoweza kujitokeza katika utani. Hivyo kwa kutumia utafiti huo ilikuwa rahisi kwa mtafiti katika kuchambua data za utafiti wake.

Vile vile, Mkubwa (2012) alifanya utafiti wenye mada “Dhima za Utani Katika Maziko na Matanga ya Wapemba na Athari Zake kwa Jamii”. Katika utafiti huo aligundua kwamba utani katika maziko ya Wapemba umeanza kuondoka kwa kiasi kikubwa. Hata hivyo jamii imekuwa ikitekeleza utani katika matanga na dhima yake kubwa ni kujiliwaza baada ya machungu ya kuondokewa. Ingawa utafiti huo, ulipingana na uhalisia wa maisha yanayoambatana na utani katika jamii ya Kojani na Kiuyu Minungwini kwa sababu hadi leo jamii hizo zimekuwa zikiendeleza utani katika maziko. Pamoja na muachano huo, utafiti huo ulikuwa na umuhimu katika kufikia malengo ya utafiti huo kutokana na mtafiti kuona namna dhima zinavyoweza kujidhihirisha katika utani.

Pia, Gora (2015) alifanya uchunguzi ambao ulijikita kuchunguza namna utani unavyofanyika katika sherehe za harusi katika jamii ya Watumbatu. Katika utafiti huo aligundua kwamba kuna aina nne za utani ufanyikao katika sherehe za Watumbatu. Nazo ni utani wa binamu, utani wa mashemeji, utani wa babu/ bibi na

wajukuu, na utani wa marafiki. Utani huo hufanywa kwa sababu ya kujitambulisha, kuonesha mahusiano, kufunza na kuburudisha. Aghalabu, utani katika jamii ya Watumbatu katika sherehe za harusi hutawaliwa na matumizi ya matusi na kejeli ambazo huwa na taashira maalumu iliyokusudiwa. Utafiti huu kama zilivyokuwa tafiti nyingine umekuwa na umuhimu kwa mtafiti kufikia lengo la utafitikwa sababu unagusia masuala ya ubainishaji wa aina za utani pamoja na matumizi ya lugha kama ilivyokuwa kwa lengo la kwanza na la pili la utafiti huu. Kwa msingi huo mtafiti alijifunza vyakutosha kuhusu vipengele hivyo.

Aidha, Othman (2015) alifanya utafiti wenye mada “Nafasi ya Utani wa Sokoni na Dikoni kwa Jamii ya Wazanzibar.” Matokeo ya utafiti huu yanaonesha kuwa utani wa sokoni na dikoni una nafasi kubwa kwa jamii ya Wazanzibari. Utani huzuka kutokana na sababu tofauti za kijamii, kiuchumi na kiutamaduni. Na hujengeka zaidi kwa maneno yenye ubeuzi dhahaka na utwezaji; na mara chache hutambwa kimatendo. Aidha, utani umekuwa ni chachu ya kuleta maelewano na udugu kwa watumiaji wa soko na dikoni na kupeleka mbele gurudumu la maisha yao. Zaidi, utafiti umegundua kuwa jadi hii bado wanajamii wanaikubali na ipo haja ya kuiendeleza kwani utani kwa wao ni kitambulisho cha utamaduni wao. Utafiti huu pia ulimpatia mtafiti kuelewa namna ya kushughulikia utafiti uliojikita katika fani ya utani. Kwa kutumia utafiti huo mtafiti alijifunza namna ya kubainisha aina za utani. Pia, kutokana na kutalii utafiti huo, mtafiti aliweza kubainisha vipengele vya lugha katika utani na dhima zinazojitokeza kwa jamii.

## **2.6 Pengo la Utafiti**

Fani ya utani ni fani kongwe katika jamii za Afrika na Tanzania kwa ujumla. Mapitio yaliyopitiwa katika sehemu hii yanaonesha kuwa tafiti kadhaa zimewahi

kufanyika zikiwa na lengo la kuchunguza utani katika jamii tofauti tofauti. Kwa upande wa Zanzibar imebainika kuwa zipo tafiti ambazo zimeuangalia utani kwa ujumla wake, na baadhi zimejikita katika kipengele cha harusi na shughuli za mazishi ama dikoni. Mapitio hayo yameonesha kuwa hadi sasa hakuna utafiti uliofanyika ukiwa na lengo la kuchunguza utani kati ya jamii ya Kiuyu Minungwini na Kojani. Hivyo, mtafiti aliona hilo ni pengo ambalo linapaswa kuzibwa. Hivyo utafiti huu ulilenga kuchunguza dhima za utani wa jadi wa jamii ya Kiuyu Minungwini na Kojani.

## **2.7 Nadharia za Utafiti**

Kwa mujibu wa Senkoro (1980) nadharia ni istilahi ya kiujumla inayomaanisha miongozo inayomwelekeza msomaji wa kazi ya fasihi kuelewa kazi hiyo ya fasihi katika vipengele vyake vyote. Kwa ujumla tunaweza kusema kuwa; Nadharia ni jumla ya maelekezo, taratibu, kanuni, misingi, mfumo uliorasmi, mwongozo na mpango unaotumiwa na msanii au mhakiki ili kumsaidia kuifanikisha au kutekeleza kazi yake ya fasihi katika hali au kiwango cha ubora au ufanisi zaidi. Katika utafiti huu, mtafiti ameongozwa na nadharia ya Simiotiki na nadharia ya Mwitiko wa Msomaji. Ufafanuzi wa nadharia hizo umefanyika kama ifuatavyo:

### **2.7.1 Nadharia ya Simiotiki**

Simiotiki ni istilahi yenye maana ya ishara. Maelezo haya yametokana na fasili za wataalam mbalimbali. Wamitila (2002), anasema kwamba Simiotiki ni neno la lugha ya Kiyunani lenye maana ya ishara na ambalo linatumika kueleza mielekeo na mikabala fulani ya kihakiki. Mikabala na mielekeo hiyo imezuka na mtindo wa kuzihakiki kazi za kifasihi ambapo unaangaza ishara aina kwa aina zilizotumika

katika kazi lengwa. Kuzuka kwa nadharia hii kunahusishwa kwa kiasi kikubwa na miaka ya 1970. Wakati huo kulikuwa na mwelekeo mkubwa wa kuuasi na kuuwacha umuundo ambao ulikuwa umeutawala uhakiki wa kifasihi katika miaka ya 1960. Hivyo, mwanaisimu wa Ki-swizi, aliyejulikana kwa jina la Ferdinand de Saussure ndie ambaye inasemekana ni mwanzilishi wa nadharia hii na aliungwa mkono na mwanafalsafa wa Kimarekani aliyejulikana kama Charles-Pierce ambaye nae anahusishwa na kielelezo cha ishara kinachohusishwa na pembe tatu ambazo ni ishara, yambwa na kifasiri. Kwa mujibu wa mwanafalsafa huyu kila ishara huwa yambwa au kitendwa kinachorejelewa.

Kifasiri ni kile kinachochochewa katika akili ya anayeifasiri ishara hiyo. Kimsingi tunaweza kusema hii ni nadharia inayoshughulika na ishara na uashiriaji katika kazi za kifasihi. Suala la ishara na uashiriaji kama anavyoelezea Culler (1970) limeanza kuwa muhimu katika uhakiki wa kifasihi.

Sambamba na hilo, pia mwanafalsafa Culler amekuwa muhakiki muhimu katika kuweka misingi mikuu ya nadharia hii. Mawazo yake pamoja na Julia Kristeva yameacha athari kubwa katika ukakiki wa ishara na uashiriaji katika kazi ya kifasihi. Dhana moja muhimu iliyohusishwa na Barthes ni msimbo. Kwa mujibu wa mawazo ya mtaalamu huyu, kila leksia hudhihirishwa misimbo au kaida fulani ambazo huwa muhimu katika kuifasiri.

### **Misimbo ya Nadharia ya Simiotiki**

Barthes (1994), anaeleza kwamba kuna aina tano za misimbo inayotumika katika kazi za fasihi ambazo kwa pamoja ndio nadharia ya Simiotiki. Aina hizo ni msimbo wa kimatukio, msimbo wa kihenemetiki, msimbo wa kiseme, msimbo wa kiishara na

msimbo wa kiurejelezi. Nadharia ya Simiotiki haiwezi kukamilika bila ya kurejelea mawazo ya Barthes kuhusu misimbo mitano ya usomaji ambao ni miongoni mwa mihimili mikuu ya nadharia hii. Mtaalamu huyu anafafanua misimbo mitano kama ifuatavyo:

**Msimbo wa Kimatukio:** Huu unahusisha jinsi msomaji anavyouunda na kuuelewa msuko wa kazi hiyo kwa kuangalia jinsi matukio hayo yanavyofuatana kiathari au kisabasishi.

**Msimbo wa Kihemenetiki:** Huu nao unahusu taharuki na unajulikana na baadhi ya wahakiki kama msimbo wa kusimulia au kutamka hadithi. Msimbo huu unaweza kufumbatwa kwenye anuani ya kazi za kifasihi.

**Msimbo wa Kiseme:** Msimbo huu unahusiana na jinsi msomaji atakavyoishia kuipata picha ya muhusika fulani wa kifasihi.

**Msimbo wa Kiishara:** Huu ni msimbo muhimu katika usomaji na uhakiki wa kazi za kifasihi. Msimbo huu unahusishwa na jinsi ambavyo wasomaji wanavyovumbua maana ya kiishara katika kazi za kifasihi.

**Msimbo wa Kiurejelezi:** Msimbo huu unajengwa kutokana na viashiria vya utamaduni unaorejelewa katika kazi inayohusika. Urejeshi huu huunda uhalisi mahususi kutokana na matumizi ya vitu fulani vinavyoeleweka na wasomaji na kwa njia hiyo huipa kazi fulani nguzo kitamaduni.

Ingawa baadhi ya watafiti kama vile Wamitila (2002) wanaeleza kwamba nadharia ya Simiotiki inachunguza zaidi vipengele vya lugha na kuvitenga vipengele vingi vya fasihi, mtafiti anaona kuwa nadharia hii inafaa katika kumfikisha kwenye lengo

la utafiti huu. Kwa sababu hiyo, mtafiti ametumia misimbo yote ya nadharia hii katika uchambuzi wa lengo la pili la utafiti huu ambalo linahusu matumizi ya lugha katika utani wa jamii zilizotafitiwa. Vile vile, katika lengo la kwanza na la tatu ameongozwa na nadharia ya Mwitiko wa Msomaji ili kuziba mapungufu ya nadharia ya Simiotiki. Hivyo nadharia hiyo ya Mwitiko wa Msomaji imefanyiwa ufafanuzi kama ifuatavyo:

### **2.7.2 Nadharia ya Mwitiko wa Msomaji**

Wafula na Njogu (2007) wanasema nadharia ya Mwitiko wa Msomaji iliasisiwa na James na wenzake katika miaka ya (1960-1970). Waasisi hawa ni Wajerumani ambao wanaamini kuwa kazi ya fasihi inapaswa kutazamwa kwa kulingana na mila, desturi na utamaduni wa msomaji. Msomaji ana uhuru wa kutafsiri kama aonavyo kutokana na uzoefu wake, na si kutokana na uzoefu wa mwandishi. Wananadharia hawa wanaweza kuwekwa katika matapo matatu ambayo ni:

- i. Wale wanaoangazia kwenye tajriba za kipekee za msomaji. Hawa ni pamoja na C. C. Lewis, (1961), Stanley Fish (1967), na Normana Holland (1968), ambao walikuwa Wamarekani.
- ii. Wale wanaofanya majaribio ya kisaikolojia kwa kikundi maalumu cha wasomaji. Hawa ni Reuven Tsur, Richarad Gerring, David Miall na Donald Kuiken
- iii. Wale wanaochukulia kwamba wasomaji wote wa kazi ya fasihi wataipokea kwa njia iliyosawa.

Hata hivyo, Stanley Fish anadai kwamba sanaa ya maneno haichanganuliwi kwa kutumia mikakati ya jaribio la kisayansi. Anayefanya jaribio la kisayansi huweka mpaka wa kihisia na kimawazo kati ya nafsi yake na jambo linalomshughulisha.

Wananadharia hao wanaeleza kuwa kazi ya fasihi inajikita katika ishara na taswira. Kutokana na ishara na taswira hizo matini za kifasihi huwa hazina maana moja bali zinakuwa na maana zaidi ya moja. Msingi mkuu wa nadharia hii ni kwamba kazi yoyote ya sanaa hurejelea kazi inayosomwa ili ithibitishwe kuwa kazi hiyo inaafikiana na yale yanayokumbukwa na msomaji wa kazi ya fasihi. Aidha, hubainisha jinsi miktadha ya matini isiyohusiana moja kwa moja na maandishi inavyoweza kuhusishwa na kutangamanishwa na msomaji.

### **Mihimili ya Nadharia ya Mwitiko wa Msomaji**

Njogu na Wafula (2007) wanasema kwamba wananadharia ya Mwitiko wa Msomaji huuliza maswali ambayo kwayo misingi ya nadharia hii imejiegemeza. Maswali hayo ni kama haya yafuatayo:

- i. Kuna uwiano wowote kati ya maana inayosomwa na jinsi msomaji anavyoihakiki?
- ii. Je, kila kazi ya fasihi ina maana kufuatana na msomaji binafsi na namna anavyoichukulia?
- iii. Kuna wasomaji ambao husoma na kufasiri kazi za fasihi vizuri zaidi kuliko wasomaji wengine.?
- iv. Msomaji hutumia vigezo gani kujijulisha iwapo mawazo yake juu ya kazi fualani yanafaa au hayafai?

Kinoti (2012) anamnukuu Adena Rosmarin katika Murfin (1999) kwa kueleza kwamba kazi ya fasihi ni kama kinyago ambacho hakijakamilika na kwa hivyo mchongaji hujaribu kukikamilisha. Kwa hivyo, Kinoti anaibainisha mihimili ya Mwitiko wa Msomaji kama ifuatayo:

- i. Msomaji huikamilisha kazi ya sanaa kwa kuijaliza kwa usomaji makini au kwa kuidhalilisha kwa usomaji wa kiholela. Iser na Fish (1967) wanadai kwamba kazi ya fasihi huwa na mapengo mengi ambayo msomaji hushurutika kutunga matini mpya amabazo zimechochewa na kuzalika kutokana na matini asili zilizoko kwenye kurasa.
- ii. Nadharia hii inasisitiza athari za kazi za fasihi juu ya akili na maarifa ya mwandishi. Wasomaji hufasiri athari hizo kupitia njia tofauti tofauti kutegemea:
  - a. Tofauti kati ya matini na hisia za kibinafsi za msomaji.
  - b. Namna matini inavyoelekeza au kutatiza mwitiko wa msomaji. Sifa inayozua usomaji mzuri ama mbaya wa kazi ya fasihi.
- iii. Wananadharia hii wanashikilia kuwa kuna njia mbili za usomaji wa kazi za fasihi ambazo ni:
  - a. Njia inayofafanua na kuisitiza mawazo ambayo kitambo yamejulikana na kutambuliwa na msomaji.
  - b. Kuwasilisha kazi ya fasihi kimapumbo ili kumchochea msomaji kujitafutia na kujiamulia ujumbe uliomo katika kazi aliyoisoma. Kwa hivyo, mafumbo hayo yanapaswa kusomwa na msomaji mara kadhaa ili kupata ujumbe uliokusudiwa.



- iv. Usomaji ni tendo linalofanywa na kutekelezwa na msomaji kwa wakati maalumu, kwamba wakati wa kusomwa kwa matini huathiri maana ya matini hiyo.
- v. Msomaji anayetumia nadharia ya Mwitiko wa Msomaji hufuata hatua tatu, ambazo ni:
  - a. Hurejelea kazi inayosomwa kwa tafsiri ili ithibitishwe kwamba kazi hiyo inaafikiana na yale yanayokumbukwa na msomaji.
  - b. Hubainisha jinsi miktadha ya matini isiyohusiana moja kwa moja na maandishi inavyoweza kuhusishwa na kutangamanishwa na msomaji.
  - c. Hudhihirisha kwamba maoni ya msomaji yanafungamana na mada muhimu za hadithi.
- vi. Nadharia hii inazingatia usomaji, msomaji na upokezi.

### **Mapungufu ya Nadharia ya Mwitiko wa Msomaji**

Wamitila (2003) anaeleza kwamba nadharia ya Mwitiko wa Msomaji ina mapungufu kutokana na kuiona kazi ya fasihi kutokuwa na maana mpaka pale inapoingia mikononi mwa msomaji. Kwa mantiki hiyo, msomaji asiyekuwa makini anaweza kuipa kazi husika maana finyu. Pamoja na ukweli huo mtafiti ameitumia mihimili ya nadharia ya Mwitiko wa Msomaji ili kumuongoza katika uchambuzi wa lengo la kwanza na la tatu la utafiti huu. Nadharia hii ilitumika ili kubainisha aina za utani na dhima za utani kama zinavyojidhihirisha katika utani wa jamii ya Kiuyu Minungwini na Kojani. Kwa kufanya hivyo, mapungufu ya nadharia ya Simiotiki yaliweza kuzibwa.

## **2.8 Hitimisho**

Sura hii inahusu mapitio ya kazi tangulizi na mkabala wa nadharia. Katika sura hii kuna sehemu ndogo ndogo ambazo ni ufafanuzi wa dhana ya utani, dhima za fasihi kwa ujumla, aina za utani, mapitio ya maandiko kuhusu utani katika makabila yanayopatikana Tanzania na mapitio ya maandiko kuhusu utani wa Zanzibar. Pia, sura hii imeonesha pengo la utafiti huu. Aidha, kuna ufafanuzi wa nadharia ya Simiotiki na nadharia ya Mwitiko wa Msomaji ambayo imeongoza utafiti huu.

## **SURA YA TATU**

### **MBINU ZA UTAFITI**

#### **3.1 Utangulizi**

Sura hii inahusumbinu za utafiti zilizotumika katika kukusanya data, kuziwasilisha na kuzichambua. Vipengele vilivyobainishwa katika sura hii ni usanifu wa tasnifu, eneo la utafiti, walengwa wa utafiti, sampuli na mbinu za usampulishaji. Pia, sura inaelezea data na mbinu za ukusanyaji wa data, uthabiti na kuaminika kwa data pamoja na maadili ya utafiti. Hivyo vipengele hivyo vimefanyiwa ufafanuzi kama ifuatavyo:

#### **3.2 Usanifu wa Utafiti**

Utafiti huu ulifanyika maktabani kwa data za upili na uwandani mtafiti alikusanya data za msingi. Data zilifanyiwa uwasilishaji na uchambuzi kwa njia ya maelezo. Mtafiti ameona kuwa njia hii ni bora kutokana na kwamba utani ni moja ya sanaa ya fasihi. Hivyo utafiti unaotumia sanaa ya maneno huwa ni muafaka data zake kufanyiwa uchambuzi na kuwasilishwa kwa njia ya maelezo. Hili linashadidiwa na Salim (2015) ambaye anaeleza kuwa tafiti za kifasihi hukidhi zaidi iwapo data zake zitatumia muundo wa kimaalezo.

#### **3.3 Eneo la Utafiti**

Enon (1998), anasema kwamba eneo la utafiti ni sehemu ambayo mtafiti hukusanya data zake za utafiti. Eneo la utafiti huu ni Kiuyu Minungwinina Kojani data za utafiti huu zilikusanywa maeneo hayo. Maeneo hayo yaliteuliwa kwa sababu utani wa jamii hiyo ulikuwa bado haujatafitiwa katika kiwango cha dhima na matumizi ya lugha.

### **3.4 Walengwa wa Utafiti**

Walengwa wa utafiti ni jumla ya watu au vitu vyote ambavyo huhusishwa katika utafiti, (Kothari, 2004, Bryman, (2004), Kombo na Tromp (2006). Hivyo walengwa wautafiti huu ni wanajamii wa Kisiwa cha Kojani na Kiuyu Minungwini ambao hushiriki katikautani wa jadi wa jamii ya watu wa Kiuyu Minungwini na Kojani katika wilaya ya Wete Mkoa wa Kaskazini Pemba.

### **3.5 Sampuli na Usampulishaji**

#### **3.5.1 Sampuli**

Sampuli ni kikundi kidogo cha watu kinachowakilisha kundi kubwa linalotafitiwa. Enon (1998) anaeleza kuhusu dhana ya sampuli kwamba ni kundi dogo la watu au vitu ambalo huteuliwa na mtafiti kwa minajili ya kuwakilisha kundi kubwa linalotafitiwa. Hivyo katika utafiti huu wateuliwa ni baadhi ya wazee, vijana na watoto ambao ni wa jamii ya Kojani na Kiuyu Minungwini.

#### **3.5.2 Usampulishaji**

Usampulishaji ni namna ya kuwapata watafitiwa wanaotoa data za utafitiunaotarajiwa kufanyika. Bryman (2004) anaeleza kwamba usampulishaji ni kitendo cha kuchagua kikundi cha vitu au watu ili kutumika katika utafiti kama kiwakilishi cha kundi lote linalotafitiwa. Mchakato huu hufanyika kutokana na ukweli kwamba si rahisi kwamtafiti kulifikia kundi lote ambalo linatarajiwa kutafitiwa. Katika utafiti huu, mtafiti alitumia usampulishaji lengwa. Huu ni usampulishaji ambao mtafiti huenda katika chanzo cha data ambacho anaamini kitampatia data za kujibu maswaliya utafiti anaoufanyia kazi. Mawazo haya yanawiana na yale ya Kothari (2014) ambaye anaeleza kuwa usampulishaji ni

kitendo cha mtafiti kwenda moja kwa moja kwenye chanzo cha taarifa ambacho mtafiti anaamini kitampatia data ambazo zitajibu maswali ya utafiti wake. Mtafiti aliamini kuwa mbinu hii ni borakatika utafiti huu kutokana na kuwa alikwenda moja kwa moja kwa wazee, vijana na watoto ambao wanafanyiana utani katika jamii ya watu wa Kiuyu Minungwini na Kojani katika Wilaya ya Wete na kupata data za utafiti huu.

#### **Jedwali la Sampuli ya utafiti**

	UMRI	WANAUME	WANAWAKE
WAZEE	72-60	10	8
VIJANA	50-35	33	21
WATOTO	16-12	16	10
JUMLA		59	39
<b>JUMLA KUU</b>			<b>98</b>

### **3.6 Ukusanyaji wa Data**

Hiki ni kipengele muhimu sana katika utafiti. Bila ya kukusanya data utafiti hauwezi kufanyika ama huweza kuwa usio thabiti. Kothari (2004) anaeleza kwamba ukusanyaji wa data ni shughuli ya kukusanya data kutoka kwa watafitiwa. Katika utafiti huu mtafiti alikusanya data za msingi na data za upili ili kukamilisha malengo mahsusi ya utafiti. Ukusanyaji wa data ulifanyika kama ifuatavyo:

#### **3.6.1 Data za Msingi**

Data za msingi ni data ambazo hokusanywa kwa mara ya kwanza kwa lengo la kufanyika utafiti. Kothari (1999) anasema kwamba data za msingi ni aina ya data ambazo hazijatumiwa na mtafiti yeyote kwa lengo la utafiti kama unaofanyika.

Victoria (2014) anataja vyanzo vya data za msingi ambavyo ni pamoja na machapisho kama vile vitabu, vitu vinavyotarajiwa kutafitiwa, watu nakadhalika. Katika utafiti huu data za msingi zilikusanywa kwa njia ya usaili kutoka kwa wazee, vijana na watoto wa jamii ya Kiuyu Minungwini na kojani.

### **3.6.2 Data za Upili**

Dhana ya data za upili inaelezwa na Panneerselverm (2012) kwamba ni jumla ya data zote ambazo zimekusanywa hapo kabla kwa matumizi ya utafiti uliowahi kufanyika. Anasema kwamba data za upili huwa na gharama nafuu, huokoa muda na hazitumii nguvu kubwa katika kuzikusanya. Naye Kothari (2004) anaeleza kwamba data za upili ni zile ambazo tayari zimekwisha kusanywa na mtafiti wa awali na ambazo zimepitia katika hatua zote stahiki za ukusanyaji data. Anaendelea kusema kwamba vyanzo vya data za upili ni pamoja na majarida, wovuti na tovuti, tasnifu mbalimbali, nakadhalika. Katika utafiti huu mtafiti alisoma majarida, vitabu, tasnifu pamoja na machapisho yanayotokana na wovuti na tovuti ili kupata data za upili ambazo zilimsaidia kufanya ushadadiaji wakati wa uchambuzi na uwasilishaji wa data za utafiti huu.

### **3.7 Mbinu za Kukusanya Data**

Utafiti wowote ule wa kisayansi hutumia mbinu mchanganyiko katika kukusanya data. Alderson (1992) anaeleza kwamba hakuna mbinu iliyobora katika utafiti ikitumika peke yake. Ni vema kukusanya data kutoka katika vyanzo na mbinu mbalimbali ili mtafiti aweze kuhakiki matokeo kupitia mbinu hizo. Kutokana na ukweli huo, mtafiti alitumia mbinu ya maktabani na mbinu ya usaili ili kupata data za utafiti huu.

### **3.7.1 Mbinu ya Maktabani**

Mbinu ya maktabani ni mbinu ya ukusanyaji data ambayo hutumiwa namtafiti kukusanya data za upili na hata zile za msingi. Kothari (2004) anaeleza kuwa mbinu ya maktabani ni mbinu ya kutalii machapisho na kupata ujumbe katika machapisho hayo kama vile vitabu, magazeti na machapisho mbalimbali ambayo mtafiti anaamini yatampatia data zinazohusina na mada ya utafiti huu. Kwa kutumia njia hii, mtafiti alikusanya data za upili ambazo zilimsaidia kubainisha tatizo la utafiti pamoja na kuandika sura ya pili ambayo inahusu mapitio ya kazi tangulizi na mkabala wa nadharia. Pia, mtafiti alitumia mbinu ya usomaji makini kutalii mifano ya utani wa jamii teule ambapo ilimuwezesha kudondoa data zilizojibu maswali ya utafiti huu. Zoezi hilo lilifanyika kwa mtafiti kunukuu data kutoka katika mifano ya utani katika shajara aliyoigawa sehemu tatu ambapo kila sehemu ilikuwa na anuani kutegemea lengo la utafiti huu.

### **3.7.2 Mbinu ya Usaili**

Mbinu ya usaili ni mbinu ya kukusanya data kwa kutumia maswali yanayoulizwa na kujibiwa kwa kutumia mdomo. Kothari (2004) anaeleza kwamba mbinu ya usaili ni mbinu ya ukusanyaji wa data ambayo mtafiti hutayarisha maswali na kuyauliza kwa mtafitiwa kwa njia ya mdomo. Mbinu hii ina kasoro kiasi fulani kutokana na kutumia muda mkubwa na gharama. Hili linathibitishwa na Enon (1998) pale anapoeleza kuwa kasoro kubwa inayoikumba mbinu ya usaili katika kukusanya data za utafiti ni kutokana na mtafiti kutumia muda mrefu na kuhitaji gharama. Hata hivyo, kwa upande mwengine ni muhimu kutokana na kutoa fursa kukusanya data kwa watu ambao hawajui kusoma wala kuandika. Hivyo pamoja na kasoro hizo

mbinu hii ilionekana ni muhimu sana katika kukamilisha utafiti huu kutokana na kwamba baadhi ya wanakiji wa Kojani na Kiuyu Minungwini ambao walimueleza mtafitiwa mifano ya utani wa jadi mwa jamii hizo hawajui kusoma wala kuandika. Hivyo mtafiti alitumia shajara na kunukuu mifano ya utani wakati wa usaili na wanajamii hiyo.

### **3.8 Usahihi, Kuaminika na Maadili ya Utafiti**

#### **3.8.1 Usahihi wa Data**

Cohen na wenzake (2000) wanasema kwamba usahihi wa mbinu za kukusanyia data ni utaratibu unaoweza kupatikana kwa data sahihi na za kuaminika za utafiti. Usahihi wa data katika utafiti huu ulihakikishwa kwa kutumia mbinu ya upitiaji wa nyaraka. Katika uchambuzi wa data, mkabala wa kinaelezo ndio ulitumika. Vile vile, usahihi wa mbinu na nadharia za uhakiki wa fasihi zilizotumika katika utafiti huu zilijadiliwa katika mjadala uliofanyika baina ya mtafiti na watafitiwa wake.

#### **3.8.2 Kuaminika kwa Data za Utafiti**

Kuaminika kwa data za utafiti kunatokana na uwezo wa mbinu za utafiti kutoa matokeo yale yale ya utafiti unaporudiwa kwa kutumia mbinu zile zile (Kothari, 2008). Katika kulifafanua hili, Furlong na Lavelace, (2000) wanasema kuaminika kwa data kunajitokeza pale ambapo kunakuwa na uhusiano au ulingano katika taarifa zinazotolewa na watu wale wale kwa muda tofauti. Katika utafiti huu, kuaminika kwa data kumhakikishwa kwa kutumia nadharia ya Simiotiki na nadharia ya Mwitiko wa Msoamaji.



### **3.8.3 Maadili ya Utafiti**

Suala la maadili ni muhimu sana katika utafiti wowote unaofanyika. Enon (1998) anaeleza kuwa maadili ya utafiti huhusishwa na tamaduni, mila na desturi ambazo jamii huziamini katika eneo ambalo mtafiti analenga kuchunguza kitu au jambo fulani. Lengo la maadili katika utafiti ni kulinda mambo ya kibinaadamu yanayoaminiwa na jamii. Pia, kuhakikisha kuwa utafiti unafanyika katika muktadha unaokubalika; kwa mtu mmoja mmoja, kikundi cha watu au jamii kwa ujumla na kuhakikisha kuwa miradi ya kiutafiti inazingatia maadili, kama vile; masuala ya uongozi na athari zake, utunzaji siri na utoaji wa habari.

Hivyo, katika utafiti huu, maadili ya utafiti yalizingatiwa ipasavyo kabla na baada ya kukusanya data. Kwasababu utafiti huu ulikuwa wa uwandani na maktabani mtafiti alihakikisha kuwa data zinakusanywa kwa usahihi kutoka kwa watafitiwa. Pia, mtafiti alichunga maadili yote ya utafiti. Vile vile wakati wa kuchambua data za utafiti huu mtafiti aliongozwa na nadharia ya Simiotiki na nadharia ya Mwitiko wa Msoamaji.

### **3.9 Hitimisho**

Sura hii imehusisha mjadala wa mbinu za ukusanyaji wa data katika utafiti huu. Sura hii inaonesha kuwa data zilikusanywa kutoka kwa jamii ya Kojani na Kiuyu Maambani. Matumizi ya mbinu hizo kama yalivyooneshwa katika sura hii yalifanikisha kupatikana data ambazo ziliwezesha kujibu maswali ya utafiti huu. Hivyo, ni wazi kuwa uteuzi wa mbinu hizi ulikuwa muafaka kwa utafiti huu.

## **SURA YA NNE**

### **UWASILISHAJI, UCHAMBUZI NA MJADALA WA DATA ZA UTAFITI**

#### **4.1 Utangulizi**

Sura hii inahusu uchambuzi wa data za utafiti. Sura imegawika katika sehemu kuu tatu kutegemeana na malengo mahususu ya utafiti huu. Sehemu ya kwanza inabainisha aina za utani wa jadi kati ya wanajamii wa Kojani na Kiuyu Minungwini. Sehemu ya pili inajadili uchunguzi wa vipengele vya lugha vinavyojitokeza katika utani wa wanajamii wa Kiuyu Minungwini na Kisiwa cha Kojani. Sehemu ya tatu imebainisha dhima za utani wa wanajamii wa Kisiwa cha Kojani na Kiuyu Minungwini. Hivyo uchambuzi wa data ulikuwa kama ifuatavyo:

#### **4.2 Aina za Utani katika Jamii ya Kojani na Kiuyu Minungwini**

Lengo la kwanza la utafiti huu lililenga kubainisha aina za utani unaojitokeza katika jamii ya Kiuyu Minungwini na Kojani. Data za utafiti huu zilionyesha kuwa jamii hizo zina aina mbalimbali za utani kutegemea miktadha ya kijamii. Kwa mfano, upo utani wa wavuvi, utani wa wanakijiji kimoja na chengine, utani wa misibani, utani wa kwenye sherehe za harusi, utani wa babu/bibi na wajukuu, utani wa marafiki na mingineyo kama inavyojibainisha katika sehemu hii.

Aina hizi za utani zimebainishwa kama ifuatavyo:-

##### **4.2.1 Utani wa Misibani**

Huu ni utani ambao hufanywa na watani wa marehemu ambaye ni mzee kati ya miaka 70 na zaidi. Utani huu huanza kufanyika mara tu baada ya kufariki marehemu, wakati wa harakati za mazishi na ndani ya siku tatu za maombolezo (matanga). Ni ada ya wanajamii hawa kuigiza matendo ama kuzungumza kama alivyokuwa

akizungumza marehemu. Moja ya mifano ya utani hii ni ule unaojitokeza kuhusu chakula alichokuwa akikipenda marehemu ambapo mtani huweza kuigiza mbele ya familia ya marehemu. Utani huu mtafiti amesimuliwa na mmoja miongoni mwa wanajamii wakongwe aliyekutana nae huko Kiuyu Minungwini alipokwa akikusanya data:

MTANI: Bibie niletee muhogo na samaki wote leo hakuna kubakisha kesho. Maana nyie kila siku wasikia nataka saza ngau cha kesho. Hapana kesho hapa. Kesho aijuaye ni Mlijuu. Kwani husikili kwamba kitoe ni kitoeo. Maanaye kiliwe leyo leyo...”

Katika dondoo hilo, mtani analenga kusawiri tabia ya marehemu ya kupenda kula samaki ambapo hakuwa anakubali kubakisha samaki hao kwa ajili ya matumizi ya kesho yake. Alikuwa anataka samaki wote waliwe siku hiyo hiyo. Mtani anapokuwa anamuigiza marehemu anakuwa yeye hachekeki anaonesha umakini mkubwa juu ya tendo analolitenda. Hata hivyo, watu wengine hufurahi kutokana na igizo hilo na hata kumsifia mtani iwapo anapatia matendo na sauti ya marehemu. Mtani anaendelea kufanya hivyo hadi pale watoto wa marehemu wanapotoa pesa kidogo ili kumzuwiamtani asiendelee.

Utani huu haujitokezi tu kwa wanaume wanapofariki lakini hata wanawake wenye rika kama hilo nao huwa ni kichocheo cha kuibuka kwa utani wa aina hii. Bibi anapofariki, watani huyaigiza matendo ya bibi huyo. Kwa mfano, huweza kumuigiza namna alivyokuwa akipenda usafi na kujiremba kama wanawake wa kisasa. Ili kuonesha tabia hiyo, mtani huweza kutafuta wanja, poda, mafuta yanayonukia na vipambo vyengine na kuigiza namna marehemu alivyokuwa akijipamba. Kwa mfano mtafiti wa kazi hii alimshuhudia mtani mmoja ambaye aliwaambia wenzake:

MTANI: Asha ncho unigaile wanja na poda yangu na kile kioo kyangu. Naona thiviyoni.

ASHA: Ha, hivyo apo (anaikiwa poda, kioo, wanja na mtani anaanza kujiremba mbele ya hadhira mara anajigeuza huku mara anajitia wanja na mafuta-vicheko vinasikika)

Aina hii ya utani hufanywa na wanaume na wanawake kutoka jamii ya Kojani na Kiuyu Minungwini. Hata hivyo kwa kiasi kikubwa iwapo marehemu alikuwamwanamme utani hufanywa mbele ya hadhira na watani wanaume. Vivyo hivyo iwapo marehemu alikuwa mwanamke utani hufanywa mbele ya hadhira na wanawake. Hii inalenga kuchunga miiko na desturi za jamii hizo ambapo utamaduni wa jamii hizo huwa hauruhusu mchanganyikoa kati ya wanaume na wanawake hasa hasa katika miktadha ya shughuli za mazishi. Kupitia Nadharia ya Mwitiko wa Msomaji iliomba fursa ya kueleza tajiriba na uzoefu anaoupata muhakiki katika jamii, mtafiti anaona kuwa jamii imekuwa ikitekeleza utani huu ingawa kuna kizazi cha sasa ambacho kimekuwa kikipinga utamaduni huo. Hata hivyo, kizazi hicho hakijafanikiwa kufifisha utamaduni huu.

#### **4.2.2 Utani katika Shughuli za Harusi**

Moja ya matukio muhimu ya kijamii katika jamii ya Kojani na Kiuyu Minungwini ni shughuli za harusi. Harusi huwakanisha watu wa kila rika wake kwa waume. Kwa vile hili ni tukio la kijamii utani huwa ni moja kati ya mambo yanayochukuliwa kuunganisha wanajamii hao. Katika sherehe ya harusi, utani huweza kufanyika kabla ya kufunga ndoa, wakati wa kufunga ndoa na hata baada ya ndoa kufungwa. Moja ya matukio ya utani ambayo mtafiti aliyashuhudia yakifanywa na wanajamii hawa kabla ya kufunga ndoa ni mwanamke kuingizwa katika singo huku watani wake wakimtongolea hivi:

“Ulivyotaka kuolewa, utampara samaki  
 Samaki ana magamba, utampara samaki  
 Bwa Mjuma ana mliowe akuruza”

Katika utani huu, mtoto wa kike anaelezwa kwa mbinu ya kutumia utani kwamba awe tayari kwa lolote linalohusu maisha ya ndoa. Kwa jamii hizi utani unalenga kumtayarisha mwanamke kuhusu suala la kufanya mapenzi na muume ambaye yeye mwenyewe tayari alikwishamchagua. Ni kutokana na sababu hiyo ndio maana anatakiwa kuwa tayari kumpokea Bwa Mjuma yaani huyo ataye funga naye ndoa. Kwa upande wa bwana harusi, watani wake hasa wanawake humchukua na kumuingiza katika singo huku wakimueleza kuwa “*kuna kijungu jikoni kimeshinda mpakuzi, hivyo yeye ndie atayekipakua. Lakini weye kazi waiweza*” Watu ambao humuingiza harusi mwanamme katika singo ni ndugu wa karibu kama vile shemegi, watoto wa mjomba ama shangazi na watani wake wengine wa ndani ya familia.

Nadharia ya Simiotiki kupitia msimbo wake wa Kiseme imetumika kufumbua fumbo lililofichwa katika wimbo uliotolewa hapo juu. Kijungu kimenasibishwa na mwanamke aliyekwisha kutayarishwa kwa ajili ya mume ambaye amekabidhiwa kisheria. Upakuzi umenasibishwa na uzinduzi anaotarajiwa kuufanya mwanamme wa kuonja tendo la ndoa kwa mara ya kwanza. Hapa ndipo watani wanapomuuliza mwanamme, ataiweza kazi hii.

Aidha, wakati wa harakati za kufunga ndoa mtafiti pia alishuhudia utani pia ukichukua nafasi yake. Mtafiti alishuhudia, wakati walii anapompa mkono mwanamme anayetaka kufungishwa ndoa, mtani huweza kuukamata yeye na kusema “*Miye ndiye muume, weye kunkujavamia tu*” hivyo muoaji huyo au ndugu alioandamana nao inapasa watoe kiasi kidogo cha pesa ili kupewa yule aliyekamata

mkono. Baada ya kupewa pesa hiyo anauacha mkono na hapo ndoa inaendelea kufungishwa.

Vile vile, baada ya ndoa kufungishwa pia mtafiti alishuhudia utani ukiendelea miongoni mwa wanajamii. Ni kawaida kusikia watani wa bi harusi wakimtania mwanamke aliyeolewa kwa kuimba “*Amtaka asingalimfuata, amtaka asingalimfuata.*” Wimbo huu huambatana na utani ndani yake unaimbwa wakati wale waliokuja kufunga ndoa wanamchukua bi harusi kutoka jamii ya Kiuyu Minungwini ama kisiwa cha Kojani.

Pia, utani huendelea hata baada ya maharusi kufika kule wanakoenda kuishi. Katika jamii hizi mashemeji wa mwanamme na watani wa mwanamme huyo huanza kumtania kwa lengo la kumkejeli mwanamke. Ni kawaida kusikika watani wakimtania bwana harusi kwa kusema “*Kuntuchukulia mke hata kufika kisimani hafiki,*” wakiwa na maana kwamba harusi huyo si mwanamke mrembo na hivyo hawakuridhika naye. Hata hivyo mwanamme anayeambiwa hivyo huwa anacheka na kufurahi kwa utani huo kwani anajua kuwa huo ni sehemu ya desturi ya jamii yao.

Kwa uzoefu wa mtafiti kama unavyodokezwa katika Nadharia ya Mwitiko wa Msomaji mtafiti amepata uthubutu wa kusema kwamba, jamii ya Kiuyu Minungwini na ile ya Kojani zinamaingiliano makubwa katika mahusiano ya ndoa. Ni vigumu kutenganisha jamii hizo kutokana na historia yake. Baadhi ya watu husema kuwa Wakojani na Wakiuyu Minungwini ni baba mmoja na mama mmoja kutokana na ndoa zao. Hivyo, wakati wa ndoa zao hujikuta wakifanyiana utani uliobeba mizaha kadhaa ndani yake.

### 4.2.3 Utani wa Kwenye Minada ya Bidhaa

Utani unaopatikana katika minada ni utani wa sokoni na dikoni. Data zilionesha kuwa katika jamii ya Kojani ndio kunapatikana utani wa dikoni kutokana na kwamba huko ndiko kunakopatikana minada inayofanyika kwenye bandari. Kwenye jamii ya Kiuyu Minungwini kwa upande wake utani huu hujitokeza pale mtu wa Kiuyu anapokwenda Kojani. Hata hivyo huko Kiuyu Minungwini uko utani wa sokoni ambako bidhaa za kawaida huuzwa. Mfano wa utani wa dikoni uliopatikana katika jamii ya Kojani wakati mwanajamii wa Kiuyu Minungwini anapokwenda Kojani ni huu:

- Dalali: (Anaanza kwa kushitua kwa kelele) “Eheeee! Wale wateja wa daga wa msumari wa bati kama walionao surualini mwao waje niwaone udume wao hapa! Haya ndoo iyo tano elfu.
- Mnunuzi: “Sita!” “Saba,” “kumi”
- Dalali: “ Andeki. Kidume msumari endautumia nyumbani kwake huyoooo!”
- Dondoo hii imetolewa na mtafitiwa mmoja huko Kiuyu Minungwini wakati alipokuwa akihojiana na mtafiti.

Mazungumzo haya yanaonesha kuwa pamoja na kwamba mazungumzo yanayofanywa kati ya dalali na mnunuzi yanalenga kufanikisha shughuli ya kibiashara inayofanyika, lakini kwa upande mwingine kuna utani ambao unafanywa na dalali ili kuwavuta wateja wake. Pamoja na utani huo mawasiliano yanaendelea bila ya hadhira yake kuonesha kukasirika na utani huo.

Hapa pana nadharia ambayo imetumika kuakisi pamoja kati ya daga wa msumari na sehemu ya siri ya mwanamme. Nadharia iliyotumika kuziakisi pamoja tabia na sifa za daga wa msumari na kile kinachomuhusu mwanamme ni ya Simiotiki kupitia msimbo wake wa kiseme ambao hueleza elementi nasibishi za kisemantiki ambapo

hutupatia picha ya muhusika fulani wa kifasihi. Dagua wa msumari wanasifa ya urefu kama ilivyosehemu ya siri ya mwanamme, ndio maana dalali akasema “dagaa msumari wa bati kama walionao surualini mwao waje niwaone udume wao hapa”. Unasibishi huu wa sifa za kisemantiki baina ya dagaa wa msumari wa bati na kilichopo kwenye suruali ya mwanamme umeletwa ili kuhamasisha jamii ya wanaume ili wasikubali kushindwa na bei elekezi inayotolewa na dalali.

Mfano mwengine wa utani katika mnada wa samaki ni maneno yanayotolewa na dalali wakati wanunuzi wanapotoa bei ya chini ambayo hajakubaliana nayo. Kwa mfano:

Dalali: “Haya papa huyunoooo lakini wengine wanapapa wao nyumbani lakini kalalie papa kwako usije ukalalia hapa?”

Wanunuzi: Hamsini, sitini.

Dalali: “Kampe mkeo hizo. Usinambie mie kuwa hutini. Mwambie akupikiaye chakula kwako...”

Wanunuzi: (Wanaendelea kutoa bei). Sabiini, moja, kumi na mbili.”

Dalali: “Kashamtaka papa huyo nambarikia andeki lete pesa ukachezee papa wako utajua mwenyewe”

Tunachokiona katika madondoo haya ni kwamba kuna utani wa hali ya juu katika minada hii ya biashara. Haya ni mazoea yaliyojengwa tangu kale na hatimae sasa imekuwa ni utamaduni wa madalali na wachuuzi kufanyiana utani huo. Othman (2015) anaeleza kuwa ni nadra sana kukuta minada ya wafanyabiashara haina utani, kwani utani katika mawasiliano ya makundi hayo ndio huchapuzi ladha ya mawasiliano kati yao. Aidha, data zilionesha kuwa huko sokoni utani pia huchukua nafasi kati ya wafanyabiashara na wateja. Kwa mfano, ni kawaida ya kusikia mazungumzo haya kati ya mchuuzi na wateja wake:

Mnunuzi: “Samaki huyu bei gani?”

Mchuuzi: “Elfu tano.”



Mnunuzi: “Tumboni ana zahabu?”

Kwa ujumla mawasilaiano haya yanautani ndani yake ambao hulenga kutokubaliana na bei iliyotolewa na mchuuzi. Mnunuzi anaposema “*Tumboni ana zahabu*” analengo la kukejeli akiwa na maana kuwa samaki huyo hafiki bei hiyo. Kejeli hii imekuja kiishara kumkejeli huyu mchuuzi kutaja bei kubwa. Kimenasibishwa na kilichopo ndani ya tumbo la samaki na dhahabu, kutokana na thamani kubwa ya dhahabu katika jamii. Hata hivyo, pamoja na kubeba kejeli ndani yake kuna kuvumiliana. Ingawa ukweli ni kwamba baadhi ya wanajamii hujikuta wakishindwa kuvumilia utani huo. Lakini wale wanaoshindwa kuvumilia wanakosolewa na wanajamii kwamba si wastaarabu. Jambo muhimu la kuzingatia ni kwamba utani hutegemea miktadha na uhusiano wa watu katika jamii. Madai haya yanaenda sambamba na madai ya Othman (2015) anapoeleza kwamba utani unaotumika katika shughuli za biashara huishia huko huko kwenye shughuli za biashara na huleta karaha iwapo utaendelezwa sehemu nyingine. Mtafiti kwa uzoefu alionao kupitia Nadharia ya Mwitiko wa Msomaji inayompa fursa ya kutoa maoni kwa vile anavyoiona kazi ya fasihi ameshawishika kueleza yale aliyoyaona kwenye masoko ya samaki na masoko ya bidhaa nyenginezo huko Kiuyu Minungwini. Huko ameyasikia na kuyaona mambo ambayo lau yangalizungumzwa kwenye jamii ya kawaida yangezua mtafaruku mkubwa sana.

#### **4.2.4 Utani wa Shughuli za Uvuvi**

Wavuvi katika jamii ya Kojani na Kiuyu Minungwini wamekuwa wakitumia utani wa hali ya juu na hata mara nyingine mtu anaweza kudhani kwamba huenda ukaibua uhasama mkubwa miongoni mwao. Kwa kawaida utani wa wavuvi hujidhihirisha

zaidi wakati wanapokuwa baharini wanavua ama kabla ya kuingia katika bahari. Mfano wa utani wa wavuvi kutoka Kojani na Kiuyu Minungwini unaojitokeza kabla ya wavuvi hao kuanza kazi yao ya kuvua ni ule unaosema hivi:

Mvuvi wa Kojani: Naona huwezi kufanya kazi mpaka uende ukapige goti “Je, nende kazini au nisende bibie.” Unamnyenyekea mkeo kama sanamu la kanisani. Hapa hatuna tu.

Mvuvi wa Kiuyu: Miye nachonga mahaba na namridhisha mke wangu si kama weye unayeridhisha vimada. Kichwa kikubwa kama cha tembo lakini akili hakina.

Huu ni mfano, wa utani unaotumiwa na wavuvi pale ambapo mmoja wao amechelewa kufika kazini. Hata hivyo, yule anayekosolewa kutokana na tabia hiyo ya kuchelewa huwa anajibu mapigo hayo kwa njia ya matani na kwa mkabala huu matani miongoni mwa wavuvi wa jamii ya Kiuyu Minungwini na Kojani inayokuwa kama ni sehemu ya mamkizi yao ambayo huambatana na kueleza uhalisia wa tabia ya mtu aliyonayo. Kwa hali hiyo utani miongoni mwao huwa ni sehemu ya utamaduni wao. Na kwa vile kundi hili hukaa pamoja na kuingiliana katika shughuli kama vile kushona nyavu, kupika, kusuka madema na kutafuta chambo hujikuta wakitumia utani kama kitambulishi cha kundi hilo. Utani huu pia huwa na malengo ya kukosoana kutokana na tabia dhaifu walizonazo miongoni mwa wavuvi. Kwa mfano hapa mvuvi mchelewaji alikuwa anasutwa kutokana na tabia yake ya kuchelewa, ila yeye alitumia fursa ya kumkosoa mwenzake aliyekuwa na tabia ya kufuga vimada.

Aidha, wavuvi wamekuwa na tabia ya kutaniana wakati wakiwa wamo baharini wanavua samaki. Kwa sababu wavuvi wa jamii ya Kojani na Kiuyu Minungwini

huwa wanavua pamoja. Watu wa familia moja kama vile baba na mtoto, babu na wajukuu, mjomba nakadhalika hujikuta ile miiko ya baadhi ya wanafamilia kama mtoto kutokumtania baba ikivunjwa kwa sababu ya kazi. Utafiti uligundua kuwa wavuvi hao wamekuwa wakiendeleza utani bila ya kuijali miiko ya utamaduni wa Waswahili ambao hauruhusu mtoto kumtania mzazi wake. Tazama mfano ufuatao:

Mvuvu wa Kojani: (Anamwambia baba yake wakiwa baharini)  
 Hooo! Kazana huko. Jikaze samaki wasiawe.  
 We ukhanisi. Jikazeeee bwege. Mvuvu Kiuyu:  
 Jaaa! Wamwambia hivyo, yule mbabayo vyooo!  
 Wantukana huna akili!

Mvuvu wa Kojani: Enyondokeya hapawe. Wee bwege wa Kiuyu,  
 miye si mtukani yeye naitukana kazi.

Kwa ujumla tunaporejelea Nadharia ya Mwitiko wa Msomaji tunachokibaini ni kwamba utani wa wavuvi umejaa dhihaka, kejeli na matusi. Mawazo haya yanalandana nayale ya utafiti wa Othmani (2015) ambao uligundua utani wa wavuvi wa Kisiwa cha Unguja hutawala muda wote na matusi, dhihaka na kejeli kama sheria kwao. Kauli kama “ukhanisi” lenye maana ya mwanamme anayefanyiwa vitendo vya ngono na “bwege” mtu aliyelegea, yote yana mkabala wa matusi katika jamii. Hii ni kusema kwamba hakuna matumizi ya lugha ya tafsida katika utani wa wavuvi.

#### **4.2.5 Utani katika Kujitambulisha**

Katika utafiti huu mtafiti amebaini kuwa utani wa utambulishi umetumika ili kuelezea jamii zilizo na chimbuko na asili moja. Wanajamii wa Kisiwa cha Kojani na Kiuyu Minungwini hutaniana kutokana na uhusiano uliopo kati yao ili kujitambulisha kwamba wanatokana na jamii moja. Jamii hizi kwa sasa zimetenganishwa na tofauti za kijografia. Inasemekana hapo kabla jamii ya Kiuyu Minungwini ilitokana na jamii ya Kojani. Hivyo jamii hizi zinapokutana haziachi

kuendeleza utani ili kujitambulisha. Mfano ngao za mikate zilizokusudiwa kupelekwa mavani huchukuliwa na kufichwa mikobani mwao. Vilevile wanajamii wa Kisiwa cha Kojani wanapokwenda Kiuyu Minungwini huwalazimisha kuwafanyia baadhi ya mambo kama vile kuwapa chakula. Wakaazi wa Kiuyu Minungwini wanapoelezwa hivyo na Wakojani husema:

WAKIUYU “Wapeni chakula wale hawajalapo hao. Wapate pumzi za kurudi kwao.”

WAKOJANI “Kama hawamiliki chakula waende Kojani kwa matajiri wakachukue kwani wao ni masikini”.

Mara nyingine utani huu huwa hata wa hatari na wa kuogopesha. Ni kawaida ya jamii hizi mbili kuchukua nyoka ama kitu ambacho hakiliwi katika jamii hiyo na kukipeleka kwa mtani wake. Kwa mfano, Mkojani anapokwenda katika jamii ya Kiuyu Minungwini huweza kuchukua nyoka ambaye amashamua na kumpeleka nyumbani kwa mtani wake huku akisema hivi:

MKOJANI: Hodi...hodi.. hodi...!

MTOTO: Karibu... Shikamoo.

MKOJANI: Marhabaa.... Wavyeleo wamo?

MTOTO: Nnn... Kankwenda chachata nguo.

MKOJANI: Basi kitoeo hicho. Kansema babayo usikiatike mpaka aje mamayo. Kwaheri.

MTOTO: Karibu.

Katika dondoo hili tunaona namna watani wanavyotumia mbinu ili kupata furasa ya kutaniana. Mkojani amejua kwamba kwa sasa mke wa mtani wake hayuko nyumbani hivyo anatumia fursa hiyo na kupeleka nyoka. Hii hufanyika baada ya kuhakikisha kwamba muume wake amemkuta sokoni au sehemu nyingine ambapo anaamini kuwa hatorudi haraka. Hivyo, mama anaporudi nyumbani inakuwa hivi:

MTOTO: Kanleta kitoweo.

MAMA: Kiwapi!

MTOTO: Nimekifunika kwenye dishi jikoni.

MAMA: (Anakwenda kukifunua tahamaki anagundua kuwa ni nyoka. Kwa msituko anasema). Jamani nyoka!...Watu wa Kiuyu hawa na utani wao!...

Pamoja na kwamba utani huu huweza kuhatarisha hisia za mtu na hata kujenga hofu lakini umekuwa ukifanyika. Yule anayetaniwa huwa hajengi chuki bali hudhamiria kulipiza kwa njia ya utani. Kwa mfano, mtu huyu aliyefanyiwa utani huu anapokwenda Kojani huamua kutekeleza utani kama sehemu ya jadi yao.

Kwa kutumia Nadharia ya Mwitiko wa Msoamaji tunabaini kuwa upo utani wa jamii ya Kiuyu Minungwini na Kojani ulio na lengo la kujitambulisha mbele ya hadhira husika. Utambulisho huo hulenga kujibainisha mbele ya wahusika wanaotoka Kojani ama Kiuyu Minungwini. Hii ni kusema kuwa watani hao huwa hawafanyi utani wenye dhima ya kujitambulisha wanapokuwa mbele ya jamii nyingine.

#### **4.2.6 Utani katika Michezo**

Jamii ya Kojani na Kiuyu Minungwini kama jamii nyingine zimekuwa na michezo yao ya jadi na ya kisasa. Michezo hiyo imekuwa ikiambatana na utani ndani yake. Mathalani, wanajamii wa kojani wamekuwa wakitaniwa pale timu yao ya mpira inapofungwa kwa kusema “Yohoo, hatunkubali kwa goli lile. Goli halifungiwa kichwa.” Au mara nyengine wanapofungwa hutaniwa hivi “Kooo! Hatukubali, hilo si goli, tan`gu lini goli kufun`giwa pembeni.” Utani huu unajitokeza kutokana na ukweli kwamba kila goli linalofungwa wanakuwa wanalitia kasoro; hawakubaliani nalo.

Kitendo cha kudai kuwa goli halifungiwi kwa kutumia kichwa au kwa upande wa pembeni ya uwanja ni kisingizio ambacho kinalenga kutaka kuchafua mchezo ambao

tayari wanaona kuwa wameshindwa na maadui zao. Hii ni kwa sababu katika kanuni za mchezo wa mpira wa miguu goli huweza kufungwa kwa kutumia kichwa ama hata kwa kutumia upande wa pembeni. Watani wanatumia mbinu hii ili kuwataka wanamichezo na washabiki wa michezo wa Kojani wasiwe na tabia hiyo ya kuzusha fujo katika michezo.

Kihistoria jamii ya Kojani kwenye mchezo wa mpira wa miguu ni watu wabishi wanaolazimisha kuzuka fujo kwenye mashindano ya mpira hasa pale wanapokuwa katika mwelekeo wa kufungwa. Jamii ya Kojanii imekuwa ikilalamikiwa kutokana na kutokubaliana na maamuzi ya waamuzi katika mpira wa miguu hasa pale timu yao inapofungwa goli na timu nyingine. Timu hiyo hufikia hata kusababisha mapigano wakati wa mashindano ya mpira wa miguu. Kwa maoni ya mtafiti kupitia Nadharia ya Mwitiko wa Msomaji inayompa fursa mtafiti kuihakiki kazi ya fasihi kwa tajiriba na uoni wake, anaona kwamba Wakojani ni watu wabishi na washindani na kwa hivyo hawakubali kushindwa kwa vyovyote.

#### **4.2.7 Utani katika Kuchumbia**

Kuchumbia ni taratibu zinazofuatwa na wanajamii wa upande wa kike na kiume ili kufanya makubaliano ya vijana wao ya kufunga ndoa yakubalike. Kwa kawaida familia ya wanaume hufunga safari kwenda kuonana na familia ya mwanamke ambaye wanamuomba fursa kufunga ndoa na kijana wao. Katika jamii ya Kiuyu Minungwini na Kojani tukio hili huambatana na utani ndani yake. Wakaazi wa Kojani wanapowaona wanaume wanaokuja kuchumbia katika jamii ya Kojani huanza kuwafanyia utani wanaume kutoka Kiuyu ambao wamekuja kumtafutia kijana wao mchumba:-

Wakiuyu Minungwini: Kojani hii hapana mke wa kumuoa hawana sifa ya kuingia mjini kwetu.

Wakojani: Hawana walijualo tukiwapeleka kwetu ni aibu tupu tutakoma kuwaokoa na maisha ya chumvi waliyonayo.

Katika dondoo hii tunaona namna utani unavyochukua nafasi katika muktadha wa posa katika jamii ya Kojani na Kiuyu Minungwini. Mazungumzo haya yamekiuka ule ukawaida wa uhalisia wa matukio ya kuchumbia katika jamii nyingi ya Kisiwa cha Pemba. Kwa kawaida watu wanapotafuta mchumba huwa wanaaheshimiana na wanakuwa hawaleti utani wenye kuchanganya matusi ndani yake. Kwa mfano, Mkojani anaposema *“tunatafuta mchumba tuoe aende akatoke safura kwa kula samaki na atakapokuja kutembea mutamuona atakavyonawiri hali yake.”* Pamoja na utani huu hakuna chuki inayojitokeza miongoni mwa watani hao wa jadi. Ama kwa upande mwengine wanawake wa Kiuyu Minungwini hujibu kwa kusema:

“Sisi hatutaki kuondolewa mjini kwetu kwenye raha ya kila kitu na kupelekwa sehemu ambayo haina hata mchanga wa kusugulia masufuria na maji matamu ya kusugulia vyombo sisi tumezowea kuosha masufuria yetu yaseme na kiambaza na mtu akipitaajione alivyo...”

Dondoo hii inaonesha kuwa hata wanawake nao huwa wanatekeleza fani hii ya utani katika jamii ya Kiuyu Minungwini katika muktadha wa posa. Kwa sababu hiyo hata wanawake wa Kojani nao huwa wanaendeleza utani katika miktadha hiyo hiyo ya posa. Kwa mfano, wanawake wa Kojani hudai kwamba hawako tayari kuolewa sehemu nyengine ambako wanawake wengi huonekana hawana afya inayoridhisha.

Mtafiti kwa uoni wake kupitia Nadharia ya Mwitiko wa Msomaji amepata fursa ya kusema kwamba uchumba unaofanywa katika jamii za Kojani na Kiuyu Minungwini hukabiliwa na utani mkubwa kutokana na utani wa asili uliokuwepo baina yao. Mara

nyingine kwa mtu ambaye hajaelewa utamaduni huo wa utani wa jamii hizo anaweza kuamini kuwa jamii hizo haziwezi kutangamana pamoja katika masuala ya ndoa. Hata hivyo, kejeli, dhihaka na maneno ya bezo yanayotolewa kwa yule anayetafuta mchumba hubakia kuwa ni maneno ya matani tu.

#### **4.2.8 Utani wa Matukio ya Ajali na Huzuni**

Wanajamii wa Kisiwa cha Kojani na Kiuyu Minungwini kama zilivyo jamii nyengine hukabiliwa na ajali mbalimbali. Tofauti ya jamii hii na jamii nyengine ni kwamba panapotokea ajali utani pia huchukua nafasi. Mfano mwanajamii wa Kisiwa cha Kojani anapofariki kwa kuanguka kutoka mitini kama mnazi, mfenesi, muembe, mshelisheli au mkarafuu watani wao hutania kwa kusema hivi:

Mkiuyu Minungwini: Ni kiasi hawawezi kukwea miti kazi yao ni uvuvi tu waoneshe ujabari wao baharini na sio juu ya miti.

Hali ni kama hiyo, pale mwanajamii wa Kiuyu Minungwini anapozama baharini akiwa katika harakati za uvuvi watani wake huchukua nafasi hiyo kwa kuanza kupitisha matani ambapo utasikia watani hao wakisema hivi:

Mkojani: Hiyo si kaziye. Haviji kuogelea na waliopo nyuma yake waache kazi ya baharini ina wenyewe wakojani la sivyo watasoza. Wacheza ngoma si yao. Hii ni kazi ya kiume.

Dondoo hili linaonesha namna jamii hizi zinavyosawiri utani hata katika matukio ambayo ni dhahiri kwamba huibua hisia za kila mwanajamii. Utafiti huu ulibaini kwamba inapotokea tanzia inayosababishwa na kifo hujaribu kukengeushwa kwa kutumia utani. Mantiki yake ni kwamba si kwamba jamii hizi huwa haziguswi na hisia hasi za tanzia hizo lakini utani unajitokeza kama sehemu ya maish yao ya kila siku.



Miktadha mingine ambayo huibua huzuni ni masuala ya kuvunjika kwa ndoa. Pamoja na kwamba suala hili linawasikitisha wanajamii wa Kojani na wale wa Kiuyu Minungwini hujikuta wakitumia utani. Kwa mfano, inapotokea mwanajamii wa Kojani alikataliwa na mke hata kama alimuoa sehemu nyingine ile basi watani wake wakisikia humuambia hivi:

Mtani: "Huwezi kukaa nae ungekuja tuita tukamchukua bila shaka humuwezi ndio maana akakukimbia na mwingine tukisikia tutamuelekeza huyo si muume rudi kwenu."

Kwa ujumla tunapoangalia utani wa jamii hizo, huku mtafiti akiongozwa na nadharia ya Mwitiko wa Msomaji tunaweza kusema kuwa matukio ya ajali na huzuni yanachukuliwa kama ni ya kawaida mno kwa kutumia mbinu ya utani. Utani huyafanya matukio hayo yawe mepesi iwapokuwa kila mwanajamii amekuwa na huzuni iliyomo moyoni kwa umbo la ndani. Kwa umbo la nje ndio hujitokeza ile furaha ya kawaida ili kuyakabili matuko hayo mazito.

#### **4.2.9 Utani katika Vyombo vya Usafiri**

Imeelezwa hapo kabla kwamba Kojani ni kisiwa kilichozungukwa na bahari ya Hindi. Ili kufika katika kisiwa hicho watu hulazimika kutumia usafiri wa vyombo vya bahari kama vile madau ama majahazi. Kwa hivyo, mtafiti amebaini kuwa watu wanapokuwa katika safari ya kuvuuka katika kisiwa hicho hujikuta wakitaniana. Mathalani, inapotokea mtu wa Kiuyu Minungwini ameingia katika dau au jahazi watani wake huanza kumtania kwa kumwambia "*Tutakuacha humu tukuone kama utafika unakokwenda.*" Wanapofika karibu na ufukweni Wakojani hujitosa baharini na kuogelea na kumuacha ndani ya dau akichukuliwa na maji.

Baada ya kitendo hicho, Wakojani huchukua muda hadi wanapoamua kwenda kumuokoa. Hili hufanyika ili wapate kuibua vicheko vya utani na karaha. Ili kujibu pigo hilo mwanajamii wa Kisiwa cha Kojani anapovuka kwenda sehemu nyengine na kukutana na watani wake huambiwa hivi:

“Wewe u mshamba kuji mjini kutafuta mahitaji yako kwani shamba haikukidhia mahitaji yako hivyo uwe makini na magari, pikipiki, vespa usije ukagongwa.”

Aidha, watu wa Kiuyu Minungwini wanapoingia katika dau na Wakojani hutaniwa kwa kuambiwa hivi:

Mkojani: “Wao ni wazito na wanaweza kusababisha kizame kwa hiyo waingie vidau peke yao wasichanganyike na Wakojani.

Mkiuyu Minungwini: “Nyie na mizigo mulionayo kutwa kucha mwasafirisha mizigo tukiingia vidauni hatuna raha ya kukaa tukaenea ni kazi hii muliokuwa hamuchoki kututa kila mukionacho mpaka mchanga wa kusugulia na viembe vichanga.”

Data hizi zinatuishirika kuwa vyombo vya usafiri ni kichocheo na chanzo kikuu cha utani miongoni mwa jamii ya Kojani na Kiuyu Minungwini. Jamii ya Kiuyu Minungwini imekuwa ikijisifia kuwa na uzoefu wa kutumia vyombo vya usafiri vya nchi kavu kama vile gari. Uzoefu huu umekuwa ukiwafanya wajisifie sana mbele ya Wakojani. Hali hii inatokana na ukweli kwamba vyombo hivi vya usafiri vya nchi kavu vinahusishwa na usasa wa maendeleo ya sayansi na teknolojia. Kwa upande mwingine, jamii ya Wakojani imekuwa ikijisifia kwa weledi wa matumizi ya usafiri wa vyombo vya baharini kama vile madau ambavyo ni vyombo vya jadi vya usafiri katika jamii hiyo.

#### 4.2.10 Utani katika Shughuli za Kilimo

Kilimo ni moja kati ya shughuli muhimu ya kiuchumi inayofanywa na jamii ya Kiuyu Minungwini na Kojani. Jamii hizi zinahistoria ya uhusiano wa koo zao. Hivyo hata sehemu wanazoshughulika na kilimo zinakuwa zimepakana. Hii ni kutokana na kwamba wengi wao wameyapata mashamba yaokwa njia ya kurithi kutoka kwa wazee wao. Hivyo kwenye taasisi hii ya kilimo pia tunakutana na utani wa jamii hizo. Moja miongoni mwa matukio ya utani kwenye shughuli ya kilimo ni ule unaofanywa na watani pale wanapoamua kumlimia shamba lake lote kwa siku moja na baadaye kumwambia:

“Ah! umvivu. Tunkufanyia hivyo ili uone watu wanavyoweza kufanya kazi kwa mara moja na sio kugongagonga.”

Hali hii hufanyika mara kwa mara na haijikiti katika kulima tu bali hata katika shughuli za uvunaji zinakabiliwa na utani miongoni mwa jamii hizo. Kwa mfano, iwapo kuna shamba la mwanajamii wa Kojani, kama vile shamba ya mpunga ambao umekuwa tayari kuvunwa. Kikundi cha watani huamua kuuvuna mpunga huo na baadae humuambia mwenyewe kuwa “*tunachukua huu ndio malipo yetu.*” Kufanya hivyo kunamfanya aliyesaidiwa kutoa shukurani.

Iwapo mpunga wao umeshaiva kwa mapenzi makubwa waliyonayo watani wao hukaa na kuuvuna hata kama ni siku moja shamba nzima baadae huchukua kiasi chao husema tunalipa nguvu zetu. Na endapo mwanajamii wa Kiuyu Minungwini katika shamba lake, mpunga wake umemea vizuri na kwa bahati mbaya jirani yake wa Kojani, mpunga wake umedumaa, basi mwenyeji wa Kiuyu Minungwini humwambia Mkojani kuwa ulipolima mara hii hukutaka ruhusa kutoka kwa mizimu yenu ya Kojani.

### **4.3 Lugha katika Utani wa Kojani na Kiuyu Minungwini**

Lengo mahususi la pili la utafiti huu lilikuwa ni kuchunguza matumizi ya lugha namna yanavyojitokeza katika utani wa jamii ya Kojani na Kiuyu Minungwini. Kwa ujumla baada ya mtafiti kuzikusanya data zinazohusu aina za utani unaotumiwa katika jamii hiyo alizitalii na kubaini kuwa utani katika jamii teule umekuwa ukitumia vipengele kadhaa vya lugha. Hivyo basi, katika sehemu hii mtafiti amefanya uwasilishaji na uchambuzi wa data zinazohusu matumizi ya lugha kama yanavyojitokeza katika utani wa jamii ya Kojani na Kiuyu Minungwini kama ifuatavyo:

#### **4.3.1 Matumizi ya Lahaja**

Lahaja ni tofauti ya matumizi ya vipengele vya lugha miongoni mwa vijilugha vinavyosemekana asili yake ni kutoka katika lugha moja. Data zilizokusanywa na mtafiti zinaonesha kuwa utani wa jamii ya Kiuyu Minungwini na Kojani umekuwa ukitumia matumizi ya lahaja hasa kilahaja cha Kojani. Hili limekuwa likifanyika kutokana na uteuzi wa maneno unaofanywa na wahusika wakati wa mawasiliano hayo. Hali hii inajitokeza katika mfano ufuatao:

Mtani: Bibie niletee muhogo na samaki wote leo hakuna kubakisha kesho. Maana nyie kila siku wasikia nataka saza ngau cha kesho. Hapana kesho hapa. Kesho aijuaye ni Mlijuu. Kwani husikili kwamba kitoe ni kitoeo. Maanaye kiliwe leyo leyo...”

Katika dondoo hilo, data zinaonesha kuwa mzungumzaji ameteua kulitumia neno “saza” ambalo lina maana ya kubakisha. Kwa kawaida neno hili hutumiwa na wazungumzaji wa kilahaja cha Kojani. Neno saza hutumika kuashiria maana yakubakisha akiba kwa ajili ya matumizi ya baadae hasa vyakula. Pia, kuna

matumizi ya neno “ngau” lenye maana ya “angalau.” Hivyo inapoelezwa kuwa “Maana nyie kila siku wasikia nataka saza ngau cha kesho”, tunapata maana kuwa mzungumzaji anapinga kitendo cha kuweka akiba ya samaki hao kwa ajili ya kesho. Mfano mwingine wa matumizi ya lahaja katika utani wa jamii hizo unajitokeza kama ifuatavyo:

Mtani: Asha ncho unigaile wanja na poda yangu na kile kioo kchangu.... Naona thivyoni.

Asha: Ha, hivyo apo (anaikiwa poda, kioo, wanja na mtani anaanza kujiremba mbele ya hadhira mara anajigeuza huku mara anajitia wanja na mafuta-vicheko vinasikika)

Katika dondoo la hapo juu, athari za kilahaja zinaonekana kujikita katika matamshi ya maneno “ncho” lenye maana ya “njoo,” “unigaile” lenye maana ya “unigaie” na “Kyahangu” lenye maana ya “changu.” Kwa ujumla kinachojidhihirisha katika mifano hii ni kwamba mzungumzaji ameathiriwa na matamshi ya kilahaja na hivyo kumfanya akengeushe matamshi ya Kiswahili Sanifu. Athari hizo za kilahaja zinazohusu uteuzi wa maneno na matamshi ndizo tunazokutana nazo wakati wanajamii wa Kiuyu Minungwini na Wakojani katika mawasiliano yao hasa yale ambayo yamekiuka miktadha iliyorasmi.

Kwa ujumla kinachobainika katika mifano hii ni kwamba baadhi ya maneno katika utani wa jamii hizo hujikita katika matumizi ya kilahaja. Hii ni kwa sababu uteuzi wa matumizi ya lugha huwa unategemea miktadha husika. Hili linaelezwa pia na Mlaga (2017) ambae anasema kuwa uteuzi wa matumizi ya maneno miongoni mwa wahusika hutegemea miktadha. Kutokana na ukweli huo ndio maana miktadha ya utani wa jamii ya Kojani na Kiuyu Minungwini imepelekea utani wa jamii teule kuteua maneno ya kilahaja ili kuendeleza utani wao.

### 4.3.2 Lugha ya Ushairi

Njogu na Chimerah (1999) wanaeleza kwamba lugha ya ushairi ina mpangilio maalumu, tofauti na maandishi ya kinathari. Data zilizokusanywa na mtafiti zimebainisha kuwa kwa kiwango kikubwa lugha ya utani wa jamii ya Kojani na Kiuyu Minungwini imekuwa ikitumia lugha ya nathari hata hivyo ipo mifano michache ya utani wa jamii hiyo ambayo imekuwa ikitumia lugha ya kishairi. Moja ya mfano wa utani unaotumia lugha ya kishairi ni ule unaosem:

Ulivyotaka kuolewa, utampara samaki  
Samaki ana magamba, utampara samaki  
Bwa Mjuma ana mliowe akuruza”

Katika dondoo hilo tunaona namna muundo wa lugha ya kishairi unavyojidhihirisha. Kwa mfano katika mshororo wa kwanza na wapili kuna kina cha mwisho cha “ki” ambacho kimeifanya mshororo hiyo kuwa na sauti ya aina moja na hivyo kuifanya iimbike. Utani huu hufanyiwa mwanamke ambaye anataka kufunga ndoa wakati wa harusi. Hivyo kikundi cha wanawake wamekuwa na tabia ya kumtania Bi. Harusi kwa kuimba wimbo huo wa utani huku wakipiga makofi kwa pamoja. Kutokana na ubeti huu tunaoneshwa namna mhusika anavyotakiwa kutii miiko ya ndoa yake kutokana na kwamba ndoa ni makubaliano ya hiari kati ya mwanamke na mwanamme yanayohalalisha maingiliano ya kimwili. Kwa hivyo ili kuyaeleza mawazo hayo, mfano huu wa utani umetumia mtindo maalumu ambao una sifa za ushairi. Sifa hizo za kishairi zinelezwa na Mdungi (2000) kwamba ni lugha ya hisi, uteuzi wa maneno na mapigo ya sauti. Uteuzi wa maneno uliotumika katika mfano huo “kumpara samaki” ambalo lina maana ya kukubali miiko ya ndoa. Mapigo ya sauti yamejengwa na sauti “ki” iliyoko mwishoni mwa mshororo wa kwanza na

wapili na hisia ni ujumbe tuupatao kutokana na utani huo. Lugha inayotumika katika sehemu kama hii ya utani inalandana na Msimbo wa Kimatukio.

### **4.3.3 Balagha**

Balagha huweza kuelezwa kama ni matumizi ya lugha yaliyokiuka uhalisia wa jambo linaloelezewa. Ndungo na Wafula (1993) wanasema kuwa matumizi haya ya lugha ni kutia chumvi. Data zilizokusanywa na mtafiti zinaonesha utani katika jamii ya Kojani na Kiuyu Minungwini umekuwa ukitumia mbinu ya matumizi ya lugha ya balagha. Kwa mfano, “Wapeni wageni umetiwa chumvi kutokana na ukweli kwamba si jambo la kawaida kwamba wale wanaoambiwa wapewe chakula hawana nguvu za kurudia nyumbani kwao hadi wale.

Mfano mwingine wa utani wa jamii ya Kojani na Kiuyu Minungwini uliotumia mubalagha ni ule unaopatikana katika miktadha ya mchezo wa mpira wa miguu. Moja ya mfano unaoonyesha mubalagha kwenye mchezo huo ni uleunaosema, “Yohoo, hatukubali kwa goli lile. Goli halifungiwa kichwa.” Wakojani wamekuwa wakitaniwa na watu wa Kiuyu kutokana na tabia yao ya kulalamikia maamuzi yanayofanywa na muamuzi wa mpira wa miguu pale timu yao inapofungwa goli. Pamoja na kwamba hiyo ni tabia ambayo imekuwa kama sehemu ya utamaduni wao lakini si sahihi kwamba timu yao inapofungwa goli kwa kutumia kichwa wamekuwa wakidai hivyo. Vile vile, katika miktadha hii ya mpira wa miguu kuna utani unaotumika uliofanana na huu ambao unasema “Kooo! Hatukubali, hilo si goli, tan`gu lini goli kufun`giwa pembeni.” Katika mfano huu pia tunaona namna utani huo ulivyotiwa chumvi kutokana na kudaiwa kuwa jamii ya Kojani haikubaliani na

maamuzi ya muamuzi wa mpira wa miguu kwa madai kuwa si sharia kushinda goli ukiwa upande wa pembeni ya goli.

Vile vile, matumizi ya chuku yanajidhihirisha katika utani unaofanywa na wanawake wa Kiuyu Minungwini. Utani huo ambao hujitokeza katika miktadha ya kufunga ndoa, wanawake wa jamii hii wamekuwa wakikataa kuolewa Kojani huku wakifanya utani unaoeleza hivi:

“Sisi hatutaki kuondolewa mjini kwetu kwenye raha ya kila kitu na kupelekwa sehemu ambayo haina hata mchanga wa kusugulia masufuria na maji matamu ya kusugulia vyombo sisi tumezowea kuosha masufuria yetu yaseme na kiambaza na mtu akipita ajione alivyo...”

Katika dondoo hilo, matumizi ya chuku yanajitokeza pale mzungumzaji anaposema “Sisi hatutaki kuondolewa mjini kwetu kwenye raha ya kila kitu na kupelekwa sehemu ambayo haina hata mchanga wa kusugulia masufuria...” Kauli hii imelenga kutia chuku kwani jamii ya Kiuyu kama zilivyo jamii nyingine za Afrika zimekuwa zikikumbwa na matatizo mbalimbali ikiwemo ya umasikini. Hivyo mzungumzaji anaposema kuwa jamii hiyo ina raha ya kila kitu analenga kukengeusha kuhusu uhalisia wa maisha ya jamii hiyo. Aidha, katika dondoo hilo matumizi ya lugha ya chuku yanajitokeza pale mzungumzaji anaposema kuwa “...kupelekwa katika sehemu ambayo haina hata mchanga wa kusugulia masufuria...” Hii pia ni chuku kutokana na kwamba Kisiwa cha Kojani kina baadhi ya sehemu ambazo ardhi yake ni mchanga. Mwisho, katika dondoo hilo la utani kuna chuku inayosema “sisi tumezowea kuosha masufuria yetu yaseme na kiambaza na mtu akipita ajione alivyo...” Maelezo haya yametiwa chumvi kutokana na kwamba masufuria hayawezi kusema na kiambaza. Pia kwa kutumia sufuria mtu hawezi kujiona, hasa masufuria



ambayo yamekuwa yakitumika kwa kupikia. Mfano mwingine wa matumizi ya chuku unajitokeza katika utani wa miktadha ya vyombo vya usafiri wa bahari.

Tazama mfano ufuatao:

Mkojani: “Wao ni wazito na wanaweza kusababisha chombo kizame kwa hiyo waingie vidau peke yao wasichanganyike na wakojani.”

Dondoo hilo hapo juu ni mfano wa utani ambao umekuwa ukifanywa ili kuwafanyia wanajamii wa Kiuyu Minungwini wakati wanapokuwa katika dau kwenda au kurudi Kojani. Kama inavyotambulika kwamba Kisiwa cha Kojani kimezungukwa na bahari ya Hindi katika pande zake zote. Hivyo ili kufika Kojani mtu inampasa atumie chombo cha kuvuuka kama vile dau. Hivyo watu wa Kiuyu wanapoingia katika madau hayo hutaniwa kwa kuambiwa kuwa watazamisha chombo hicho kutokana na uzito walionao. Hata hivyo, ukweli ni kwamba hiyo huwa ni chuku tu kwa vile huwa hawana uzito wa kukizamisha chombo wanachosafiria kutokana na uzito walionao.

Matumizi ya lugha ya chuku pia hutumiwa na Watu wa Kiuyu Minungwini ili kusawiri harakati za maisha ya hapa na pale ya wanajamii wa Kojani. Kutokana na harakati hizo kuna utani huu ufuatao:

Mkiuyu Minungwini: “Nyeie na mizigo muliyonayo kutwa kucha mwasafirisha mizigo tukiingia vidauni hatuna raha ya kukaa tukaenea ni kazi hii muliokuwa hamuchoki kututa kila mukionacho mpaka mchanga wa kusugulia na viembe vichanga.”

Katika mfano huo wa utani kuna matumizi ya chuku pale mzungumzaji anaposema “Nyeie na mizigo muliyonayo kutwa kucha mwasafirisha mizigo.” Hii ni balagha kutokana na ukweli kuwa watu wa Kojani hawasafirishi mizigo usiku na mchana

wote. Pili, mzungumzaji anaposema "...hamuchoki kututa mukionacho..." Kauli hii pia imetumika kuibua chuku ndani yake kutokana na ukweli kwamba mtu hawezi kuchukua kila kitu anachokiona. Hapa msemaji anakusudia kuonesha namna Wakojani wanavyosafiri kuelekea kwenye kisiwa cha Kojani huku wakiwa wamechukua mahitaji yao ya kijamii kama vile vyakula ambavyo wamenunua au wamevuna nje ya Kisiwa hicho.

Kwa ujumla matumizi ya lugha ya chuku katika utani wa jamii ya Kojani na Kiuyu Minungwini umekuwa ukitumika ili kusisitiza kile wanachomueleza mhusika. Hivyo dhima hii ya msisitizo inayojitokeza katika utani wa jamii hizo ndiyo inayoelezwa na Ndungo na Wafula (1993) kwamba maneno katika lugha ya chuku huwa yamechaguliwa kwa uangalifu ili kuibua hisia yasisitize au kupeleka funzo lililokusudiwa katika jamii husika.

#### **4.3.4 Kejeli**

Hii ni mbinu ambayo humdunisha mtu. Ndungo na Wafula (1993) wanaeleza kuwa kejeli ni matumizi ya lugha kwa lengo la kumdharau, kumchekelea au kumfanyia mzaha mtu. Data zilizokusanywa zinaonesha kuwa utani wa jamii ya Kojani na Kiuyu Minungwini umekuwa ukitumia lugha ya kejeli. Tazama mifano ifuatayo:

Mnunuzi: "Samaki huyu bei gani?"

Mchuuzi: "Elfu tano."

Mnunuzi: "Tumboni ana zahabu?"

Katika dondoo hilo hapo juu, mnunuzi anatumia kejeli anaposema "*Tumboni ana zahabu?*" Kauli hii inalenga kukejeli bei aliyopewa na mchuuzi akionesha kwamba samaki huyo hafiki bei hiyo, labda angekuwa ana dhahabu. Vile vile, kejeli inajitokeza pale wanajamii wanapomwambia Bwana harusi "Kuntuchukulia mke

hata kufika kisimani hafiki.” Picha inayopatikana kupitia kejeli hii ni kwamba Bwana harusi amefunga ndoa na mwanamke asiekuwa mrembo. Kwa sababu hiyo huambiwa kuwa hata kisimani hafiki.

Mfano mwingine wa kejeli katika utani wa jamii ya Kojani na Kiuyu Minungwini unajitokeza hivi; *“Wapeni chakula wale hawajalapo hao. Wapate pumzi za kurudi kwao.”* Katika utani huu watu wa Kojani hukejeliwa kwa kuambiwa kwamba hawajawahi kula chakula hivyo hawana nguvu za kurudia nyumbani hadi pale watapopewa chakula. Aidha, utani wenye kubeba kejeli unajitokeza katika miktadha ya wanajamii wa Kiuyu Minungwini wanapokwenda Kojani kutafuta mchumba wa kufunga naye ndoa. Kejeli hiyo inajitokeza hivi:

Wakiuyu Minungwini: Kojani hii hapana mke wa kumuoa hawana sifa ya kuingia mjini kwetu.

Katika dondoo hilo jamii ya Kiuyu Minungwini inakejeli wanawake wa Kojani kwa kudai kwamba hawana sifa ya kuolewa na kupelekwa katika kijiji cha Kiuyu Minungwini. Aidha, utani mwingine wenye kubeba kejeli katika miktadha ya kutafuta mchumba wa kufunga nae ndoa unasema *“Hawana walijualo tukiwapeleka kwetu ni aibu tupu tutakoma kuwaokoa na maisha ya chumvi waliyonayo”*. Pamoja na kejeli hii baadaye wanafunga ndoa na wanawake hao. Hii ni kwa sababu kile kinachozungumzwa kama kejeli huwa hakina uzito katika matendo yao. Kwa upande mwingine watu wa Kojani wanapokwenda kutafuta mke.

Vile vile, matumizi ya lugha ya kejeli yanajitokeza katika miktadha ya minada ya samaki. Kejeli hizo hutolewa na dalali wakati anaponadisha samaki. Angalia mfano unaofuata ambao ni mazungumzo ya mnadani kati ya dalali wa samaki na wachuuzi kama ifuatavyo:

- Dalali: “Haya papa huyunooooo lakini wengine wanapapa wao nyumbani lakini kalalie papa kwako usije ukalalia hapa?”
- Wachuuzi: Hamsini, sitini.
- Dalali: “Kampe mkeo hizo. Usinambie mie kuwa hutini. Mwambie akupikiaye chakula kwako...”

Katika dondoo hilo, dalali anawakejeli wachuuzi kwa kutumia nafasi ya samaki aina ya papa ambaye alikuwa anamnadisha. Dalali anaposema “*lakini wengine wana papa wao nyumbani*” anamaanisha wana wake zao ambao anawafananisha na papa. Kwa mwanamke kufananishwa na papa ni kejeli ambayo inalenga kumdunisha mwanamke huyo na kuonekana kuwa hana thamani. Kwa sababu baadhi ya jamii hawatumii samaki huyu na hata wale wanaotumia anauzwa kwa bei ya chini ukilinganishwa na samaki wengine katika mabandari na masoko.

#### **4.3.5 Dhihaka**

Dhihaka ni tamathali ya usemi ambayo inadhamiriwa kugusa hisia ya mtu kwa njia ya waziwazi na aghalabu kwa njia ya kufichua ubaya fulani au udhaifu alionao mhusika fulani (Senkoro, 1982 na Wamitila, 2003). Kimsingi dhihaka hukusudiwa kuchochea hisia za ndani za anayeambiwa. Mara nyingi, dhihaka hukusudiwa kumtweza au kumuumiza mtu. Huwa ni aina ya usemi ambao una uchungu na kero na ni aina ya kejeli ambayo ina dhamira mbaya. Data zilizokusanywa na mtafiti zinaonesha kuwa utani katika jamii ya Kiuyu Minungwini na Kojani umekuwa ukitumia dhihaka. Tazama mfano ufuatao ambao mtafiti alishuhudia mwanajamii mmoja akimwambia mwenziwe kwamba, “Wewe u mshamba kuji mjini kutafuta mahitaji yako kwani shamba haikukidhia mahitaji yako hivyo uwe makini na magari, pikipiki, vespa usije ukagongwa.”

Katika dondoo hilo hapo juu, data inaonesha kuwa neno “*mshamba*” limetumika ili kudhihaki wanajamii wa Kojani ambao hawana uzoefu na vyombo vya moto kama vile gari. Kwa sababu hiyo wanaonekana kuwa hawana uzoefu na sheria za barabarani. Katika kujibu utani huo, pale Wakojani wanapopata nafasi huwatania Watu wa Kiuyu Minungwini hivi:

Mkojani: Hiyo si kaziye. Haviji kuogelea na waliopo nyuma yake waache. Kazi ya baharini ina wenyewe Wakojani la sivyo watasoza. Wacheza ngoma si yao. Hii ni kazi ya kiume.

Katika dondoo hilo, tunaona namna Mkojani anavyowadhiki watu wa Kiuyu Minunwini kutokana na kutoweza kuogelea. Utani huu mara nyingi hutumiwa wakati wavuvi wanapokufa maji. Ikitokea mtu kafariki basi wale waliobakia hutahadharishwa kwa kutumia mfano huu wa dhihaka. Dhihaka pia hutumiwa na wavuvi wakati wanaposubiriana ili kuelekea baharini. Mfano wa dhihaka hiyo ni kama ifuatayo:

Mvuvi wa Kojani: Naona huwezi kufanya kazi mpaka uende ukapige goti “Je nende kazini au nisende bibie.” Unamnyenyekea mkeo kama sanamu la kanisani. Hapa hatuna tu.

Mvuvi wa Kiuyu: Miye nachonga mahaba na namridhisha mke wangu si kama weye unayeridhisha vimada. Kichwa kikubwa kama cha tembo lakini akili hakina.

Katika dondoo hilo, tunaona namna jamii hizo zinavyodhihaki kutokana na uhusiano wa mapenzi kati ya mke na mume. Mkojani anadhikiwa na kuonekana hana thamani kutokana na kutaka ruhusa kwa mkewe, pale anapotaka kwenda kazini. Kitendo hicho kinaonekana hakina maana na ni cha kumdunisha mwanamme. Mkiuyu naye anadhiki Mkojani kutokana na kitendo cha ngono holela. Kitendo

hicho kinamfanya aonekane kuwa ni mtu asiye na akili. Katika miktadha hii ya mapenzi na ndoa pia kunajitokeza utani uliobeba dhihaka kama ifuatavyo:

Mtani: “Huwezi kukaa nae ungekuja tuita tukamchukua bila shaka humuwezi ndio maana akakukimbia na mwengine tukisikia tutamuelekeza huyo si muume rudi kwenu.”

Katika dondoo hilo tunaona namna mhusika aliyekimbiwa na mkewe anavyodhihakiwa. Tunaona jinsi anavyoonekana kuwa hana uwezo wa kuishi na mwanamke ndio maana ameshindwa kumdhibiti nyumbani. Kwa ujumla dhihaka kama hizi zimetawala sana miongoni mwa wanajamii husika. Hata hivyo, kunakuwa na uvumilivu miongoni mwa wahusika.

#### **4.3.6 Lugha ya Matusi**

Sifa nyingine ya matumizi ya lugha katika utani wa jamii ya Kojani na Kiuyu Minungwini ni kwamba lugha yao inatumia misamiati ambayo inabeba matusi ndani yake. Hii ni kutokana na kwamba utani wa jamii hizo umekuwa ukifanywa na watu wenye uhusiano wa karibu katika harakati za maisha ya kila siku. Hili linadhihirika katika dondoo lifuatalo. Mtafiti alipokuwa akikusanya data zake, huko bandarini kisiwani Kojani, alisikia harakati za mnada zikiendelea kama hivi:-

Dalali: (Anaanza kwa kushitua kwa kelele) “Eheeee! Wale wateja wa dagaa msumari wa bati kama walionao surualini mwao waje niwaone udume wao hapa! Haya ndoo iyo, tano elfu.

Mnunuzi: “Sita!” “Saba,” “kumi”

Dalali: “Andeki. Kidume msumari endautumia nyumbani kwake huyooooo!”

Katika dondoo hilo kuna matumizi ya neno “msumari wa bati” ambalo linatupa picha ya kiungo cha uzazi cha mwanamme. Dalali anaamua kutumia lugha hiyo yenye matusi ndani yake bila kujali athari zake. Lugha hiyo ya matusi inazidi

kuendelezwa na dalali katika dondoo la hapo juu pale anaposema “Andeki. Kidume endautumia nyumbani kwake huyooooo.” Kwa kutumia kauli hii mzungumzaji anazungumzia uhusiano wa maingiliano ya kimwili kati ya mtu na mke wake. Ingawa katika jamii ya Kiuyu Minungwini na Kojani kuzungumzia uhusiano huo hadharani ni mwiko ambao huweza kusababisha migongano miongoni mwa wahusika, lakini katika miktadha ya utani inaonekana ni jambo la kawaida. Mfano mwingine wa utani ambao umebeba lugha ya matusi katika jamii ya Kojani na Kiuyu Minungwini unajitokeza katika miktadha ya uvuvi kamaifuatavyo. Mtafiti alisimuliwa na mtafitiwa kuwa katika miktadha huu, mtoto anaweza kumtukana hata baba yake mzazi, katika njia za utani.

Mvuvu wa Kojani: (Anamwambia baba yake wakiwa baharini) Hooo!  
 Kazana huko. Jikaze samaki wasiawe. We  
 ukhanisi. Jikazeeee bwege.  
 Mvuvu Kiuyu:Jaaa! Wamwambia hivyo, yule mbabayo vyooo!  
 Wamtukana huna akili!  
 Mvuvu wa Kojani: Enyondokeya hapawe. Wee bwege wa Kiuyu,  
 miye si mtukani yeye naitukana kazi.

Kwa ujumla katika utani wa Kiuyu Minungwini na Kojani mara nyingine kunatumiwa lugha yenye matusi. Ingawa kwa kiasi kikubwa utani huo huwafanya wahusika wavumiliane kutokana na mazoea na uhusiano walionao. Hii ni athari hasi ambayo inajidhihirisha katika utani wa jamii nyingi ulimwenguni. Mawazo haya yanafanana na yale ya Othman (2015) ambaye anaeleza kuwa utani unatumia lugha ambayo huondoa heshima ya baadhi ya watu kutokana na kutumika lugha ya matusi ndani yake. Anaendelea kueleza kuwa pamoja na kuwa kauli hizo huonekana kuwa lugha iliyokubalika katika jamii husika lakini bado sifa ya kuwa ni kauli za kuvunjiana heshima hubakia pale pale.

Uzoefu na tajiriba alizonazo mtafiti kupitia Nadharia ya Mwitiko wa Msomaji inayompa fursa mtafiti kuihakiki kazi ya fasihi kutokana na uzoefu na tajiriba aliyonayo mtafiti amewahi kuwashuhudia watu wa Kiuyu Minungwini na Kojani wakitaniana utani wenye matusi, bila kuona kwamba jambo hilo linaweza kuleta ukakasi baina ya wale wanaostahiana. Matusi kama hayo katika muktadha wa kawaida hayana nafasi katika jamii hizi, ila hutekelezwa bila mashaka kwenye maeneo kama uvuvini na kwenye sehemu za shughuli kama hizo.

#### **4.4 Dhima za Utani wa Jadi wa Jamii ya Kojani na Kiuyu Minungwini**

Lengo mahususi la tatu la utafiti huu lilikuwa ni kubainisha dhima za utani wa jamii ya Kiuyu Minungwini na Kojani. Ili kufikia lengo hilo mtafiti alizitalii data za utafiti na kuziwasilisha. Baada ya kuziwasilisha alizichambuana kwa njia ya maelezo. Data hizo zilionesha kuwa utani wa jadi katika jamii ya Kiuyu Minungwini na Kojani una dhima kama ifuatavyo:

##### **4.4.1 Kukuza Lugha**

Taasisi ya Ukuzaji Mitaala (1988) wanaeleza kuwa lugha ni njia ya mawasiliano kwa kutumia maneno. Hivyo mawasiliano ya binadamu yanayoweza kuitwa lugha ni yale tu yanayotumia maneno. Matumizi ya maneno hutegemea miktadha mahususi. Hivyo data zilizokusanywa na mtafiti zinaonesha kuwa utani baina jamii ya Kiuyu Minungwini na Kojani ni miongoni mwa njia ya kukuza lugha ya Kiswahili kutokana na kuibua misamiati ambayo hukitajirisha Kiswahili. Hili linathibitishwa katika mifano ifuatayo:

Mtani: Bibie niletee muhogo na samaki wote leo hakuna kusaza kesho. Maana nyie kila siku wasikia nataka saza ngau cha kesho. Hapana kesho hapa. Kesho aijuaye ni Mlijuu. Kwani



husikili kwamba kitoe ni kitoeo. Maanaye kiliwe leyo leyo...”

Katika dondoo la hapo juu, kuna matumizi ya neno “kusaza” lenye maana ya kuweka akiba. Aidha, neno “ngau” lina maana ya “angalau” na neno “Mlijuu” lina maana ya Mwenyezi Mungu.” Mbinu hii imesaidia sana kuingiza maneno mapya katika lugha ya Kiswahili ingawa hadi sasa maneno hayo hayajawa Kiswahili rasmi lakini katika lahaja ya Kojani yamekuwa yakitumika kama chombo cha mawasiliano. Mfano mwingine wa utani ambao una dhima ya kukuza lugha ya Kiswahili unajitokeza hivi:

Dalali: “Haya papa huyunooooo lakini wengine wanapapa wao nyumbani lakini kalalie papa kwako usije ukalalia hapa?”

Katika dondoo hilo, kuna matumizi ya neno “papa” ambalo limetafsiriwa na BAKIZA (2010) kuwa ni samaki mkubwa wa baharini mwenye mapezi anayezaa watoto na ambaye meno yake yanaota tena yanapong`oka. Pamoja na maana hii, neno papa katika dondoo hilo limetumika likiwa na maana ya ziada likiwa na maana ya kiungo cha uzazi cha mwanamke. Kutokana na maana hii ndio maana dalali anasema kuwa “wengine wana papa wao nyumbani.”

Kwa ujumla uibuaji wa maneno katika utani wa jamii ya Kiuyu Minungwini na Kojani ni kiungo muhimu cha kukuza lugha. Kwa kutumia Nadharia ya Simiotiki kupitia msimbo wake wa Kiseme unaonasibisha elementi za kisemantiki baina ya vitu viwili, mtafiti hapa amenasibisha papa na kiungo cha siri cha mwanamke kutokana na tabia ya viwili hivi kuwa na tabia ya kutoa harufu vinapoachwa bila kushughulikiwa. Papa kama hakushughulikiwa na kutunzwa anaweza kutoa harufu ya karaha, kama kinavyoweza kufanya kiungo cha siri cha mwanamke kisipotunzwa.

Tunaporejelea nadharia ya Mwitiko wa Msomaji inayompa fursa mtafiti kuhakiki kazi ya fasihi kutokana na tajiriba na uzoefu wa mambo anaouona katika jamii yake, mtafiti amepata fursa ya kutoa maoni yasemayo kuwa utani wa jamii ya Kiuyu Minungwini na Kojani huibua misamiati ambayo hutumika katika mawasiliano yanayotumia lugha ya Kiswahili. Kwa sababu hiyo, katika utafiti huu mtafiti anaweza kuhitimisha kwa kusema kuwa fani ya utani katika jamii teule ni kichocheo cha ukuzaji wa lugha ya Kiswahili.

#### **4.4.2 Kuendeleza Utamaduni**

Utamaduni ni jumla ya mila, desturi na silka za jamii husika. Khamisi (2008) anafafanua dhana ya utamaduni kwa kusema kuwa utamaduni ni maisha ya mtu au jamii katika mazingira maalumu ya asili yanayojumuisha lugha mama, imani, mila, desturi, maadili, itikadi, sanaa, michezo na mazingira yao. Kila fasihi husawiri utamaduni wa jamii husika. Hivyo basi, data zilizokusanywa kutokana na utani wa jamii ya Kojani na Kiuyu Minungwini zinaonesha kuwa matumizi ya utani yanasawiri utamaduni wa jamii hizo. Tazama mfano wa utani unaofanywa na jamii hizo wakati wa misiba. Aina hii ya utani mtafiti alielezwa na mwanajamii alipokuwa akikusanya data zake kwenye eneo lake la utafiti. Utani wenyewe hufanywa kama hivi:-

- Mtani: Asha ncho unigaile wanja na poda yangu na kile kioo kyangu.... Naona thiviyoni.  
 Asha: Ha, hivyo apo (anaikiwa poda, kioo, wanja na mtani anaanza kujiremba mbele ya hadhira mara anajigeuza huku mara anajitia wanja na mafuta-vicheko vinasikika).

Katika dondoo hilo, data inaonesha kuwa jamii ya Kiuyu Maambani ina utamaduni wa kufanyiana utani wakati wa matukio ya misiba. Wakati wa misiba pia, wajukuu

na watani wengine wa marehemu huwa wanaigiza matendo aliyokuwa akiyafanya marehemu. Tukio hilo hupunguza machungu ya wafiwa. Tukio kama hili linaenda sambamba yaleyale yaliyoelezwa na Ogacho (1974) pale aliposema kuwa utani wa aina hii umeanza tangu wakati marehemu yuko hai na huendelezwa hata baada ya kifo chake. Utani huo huendelea mpaka wazee watoe pesa. Kwa mfano, katika jamii za Uswahilini wajukuu huweza kudai mchele ili wafanyiwe bumbwi wakishapewa basi watatwanga huku wakimuigiza marehemu wakati wa uhai wake.

Utamaduni mwengine unaojitokeza katika utani wa jamii teule ni ule wa jamii nzima kushirikiana katika tukio la harusi kama sehemu ya tukio la kijamii. Mutembezi (2012) anaeleza kwamba tukio la kijamii ni tukio ambalo huwakanisha wanajamii kwa pamoja. Tazama wimbo wa utani unaowakushanya wanajamii hiyo:

“Ulivyotaka kuolewa, utampara samaki  
Samaki ana magamba, utampara samaki  
Bwa Mjuma ana mliowe akuruza”

Wimbo huu ambao hutumika kama sehemu ya utani huimbwa na wanajamii kwa pamoja ili kumuambia biharusi, wakati wa kufunga ndoa. Wimbo huo unalengo la kumtaka mwanamke awe mvumilivu na akubali kuishi maisha ya ndoa kama alivyokwisha kubali hapo kabla. Anapoelezwa kuwa “Samaki ana magamba, utampara samaki” ni utani wenye kuelezwa kwa njia ya tafsida yenye maana ya kwamba avumilie katika suala zima la maingiliano ya kimwili.

Tunaporejlea Nadharia ya Mwitiko wa Msomaji mtafiti amebaini kuwa kila mwanajamii katika jamii ya Kojani na Kiuyu Minungwini amekuwa akishiriki katika utani ambao huonesha utamaduni wa jamii hiyo. Imekuwa ni jadi ya jamii hizo kufanyiana utani wakati wa misiba ya vifo vya wapendwa wao. Hata hivyo, utani

huo hauwezi kuchukua nafasi katika jamii hizo pale anapofariki kijana au mtoto. Nafasi ya utani wa msibani hufanyika anapokufa mwanamme au mwanamke ambaye amezidi umri wa miaka sitini. Aidha, nyimbo za utani ni moja kati ya nyimbo ambazo hutumiwa na jamii hizo katika maswali ya kijamii kama chuo cha kuwafundisha wanandoa.

#### 4.4.3 Kukuza Fasihi ya Kiswahili

Fasihi ni sanaa itumiayo lugha ili kufikisha ujumbe unaokusudiwa. Mulokozi (1996) anakibainisha kipera cha utani kama sehemu ya fasihi ya mazungumzo ambayo ina vitanzu kama hotuba, malumbano ya watani, mizaha na sala. Fani hii huwa na kanuni zake, miktadha yake na mipaka yake katika jamii inayohusika. Hivyo basi, data zilizokusanywa na mtafiti zinaonesha kuwa utani unajidhihirisha kuwa ni sehemu ya sanaa ya fasihi ya mazungumzo. Tazama mifano ifuatayo:

“Ulivyotaka kuolewa, utampara samaki  
Samaki ana magamba, utampara samaki  
Bwa Mjuma **ana mliowe akuruza**”

Katika dondoo la hapo juu, tunaona mfano wa ubeti wa ushairi. Hata hivyo, ushairi huo umetumika kama sehemu ya utani kati ya wanajamii na biharusi. Ushahidi huo unatupelekea tuamini kuwa utani wa jamii ya Kojani na Kiuyu Minungwini ni moja kati ya fani ya fasihi ambayo inaitajirisha fasihi ya Kiswahili. Mfano mwingine wa utani unajidhihirisha kupitia malumbano ya watani. Tazama mfano ufauatao:

**Mvuvi wa Kojani:** (Anamwambia baba yake wakiwa baharini)  
Hoo! Kazana huko. Jikaze samaki wasiawe.  
We ukhanisi. Jikazeeee bwege.  
**Mvuvi Kiuyu:**Jaaa! Wamwambia hivyo, yule mbabayo vyooo!  
Wamtukana huna akili!  
**Mvuvi wa Kojani:** Enyondokeya hapawe. Wee bwege wa Kiuyu,  
miye si mtukani yeye naitukana **kazi**.

Katika data iliyopo hapo juu, tunaona namna wahusika wanavyofanyiana utani. Huu ni utani ambao unaweza kuwekwa katika tapo la utani wa marafiki. Hili ni moja ya aina ya utani anaoubainisha Mulokozi (1996) ambapo aina nyingine za utani ni pamoja utani wa mababu, mabibi na wajukuu. Utani wa mashemeji, utani wa kikabila. Vile vile, utani unajitokeza kama sehemu ya fasihi kutokana na mfano ufuatao:

Dalali: “Haya papa huyunoooo lakini wengine wanapapa wao nyumbani lakini kalalie papa kwako usije ukalalia hapa?”

Katika dondoo hilo, kuna taswira ya “papa,” inayopatikana pale dalali anaposema “wengine wana papa wao nyumbani...” Picha iliyojengewa kupitia taswira hii ni ile ya mwanamke katika miktadha ya kufanya mapenzi. Hata hivyo, mzungumzaji anatumia lugha ya taswira ili kuepuka kuzungumza kwa lugha ya wazi masuala ya maingiliano ya kimwili. Kulingana na mawazo haya Khamis (2002) anaeleza kuwa fasihi ikiwemo nyimbo hutumia lugha iliyo na mafumbo ili kuepuka matusi ya wazi kuambatana na mila na desturi za Waswahili. Hivyo miiko hiyo ndiyo tunayokutana nayo katika baadhi ya mifano ya utani wa jamii teule.

Matumizi haya ya utani kama sehemu ya fasihi ya Kiswahili miongoni mwa jamii ya Kiuyu Minungwini na Kojani yanaakisiana moja kwa moja nadharia ya Mwitiko wa Msomaji. Kwa kutumia nadharia iliyompa mtafiti fursa ya kuihakiki kazi ya fasihi kwa uoni wake kutokana na tajiriba aliyonayo, mtafiti amebaini kuwa jamii hizo zimekuwa zikitumia fani ya utani katika nyanja mbalimbali za maisha. Hii humfanya kila mwanajamii kutumia fasihi ya utani. Hata hivyo utani hufanyika kutegemea uhusiano baina ya wahusika. Kwa mfano, ni mwiko katika jamii ya Kojani na Kiuyu Minungwini kumtania baba, mama, ami, nakadhalika. Ndio maana

iwapo mtu atajisahau na kumtania mtu asiyekuwa mtani wake huambiwa “Mimi si mtani wako, kamwambie mama yako akupe mtani wako.” Hapo anatahadharishwa mtu kumtania mtu asiyekuwa mtani wake.

#### 4.4.4 Kutambulisha

Dhima nyingine ya utani wa jamii ya Kojani na Kiuyu Minungwini ni ile ya kuitambulisha hadhira. Data zilizokusanywa zinaonesha kuwa wanajamii wamekuwa wakitumia fani ya utani ili kujitambulisha wakati wanapokutana. Kwa mfano, Wakojani na Kiuyu Minungwini wanapokutana hutumia utani ili kutambulisha uhusiano wao. Tazama mfano ufuatao ambao umekuwa ukitumika katika muktadha wa msibani:

Mtani: **Bibie** niletee muhogo na samaki wote leo hakuna kubakisha kesho. Maana nyie kila siku wasikia nataka saza ngau cha kesho. Hapana kesho hapa. Kesho aijuaye ni Mlijuu. Kwani husikili kwamba kitoe ni kitoeo. Maanaye kiliwe **leyo leyo...**”

Dondoo hili linatudokeza kwamba watu wa jamii hiyo wamekuwa wakitumia utani kama sehemu ya utamaduni wao wa kujitambulisha na kuonesha uhusiano kati ya marehemu na ndugu wa marehemu. Ingawa katika dondoo hilo marehemu anakosolewa kutokana na tabia yake ya kukataa kuweka akiba. Kwa upande mwingine mhusika anajitambulisha kuwa anauhusiano na marehemu. Kitendo hiki huifanya hadhira iulize “*kwani ni nani yake yule?*” Swali hilo huulizwa kwa sababu si kila mwanajamii ana nafasi ya kufanya utani katika misiba ya jamii hizo. Mara nyingi babu, bibi na wajukuu ndio huchukuwa nafasi hiyo. Tazama mfano mwingine hapo chini:

- Mtani: Asha ncho unigaile wanja na poda yangu na kile kioo kchangu.... Naona thiviyoni.
- Asha: Ha, hivyo apo (anaikiwa poda, kioo, wanja na mtani, anaanza kujiremba mbele ya hadhira mara anajigeuza huku mara anajitia wanja na mafuta-vicheko vinasikika).

Katika dondoo hilo, watani wanashuhudiwa jinsi wanavyofanya igizo kuhusu maisha ya marehemu katika miktadha ya msibani. Mhusika mmoja anachukuwa uhusika wa bibi na mhusika mwingine anachukuwa nafasi ya kuwa mjukuu. Igizo hili pia linawatambulisha wahusika mbele ya hadhira. Ni wazi kwamba huu ni utani kati ya bibi, babu na wajukuu. Dhima hii ya utani imekuwa ikijitokeza katika makabila mengi hapa Afrika. Hili linafafanuliwa pia na Mulokozi (1996) anapoeleza kwamba mila ya utani imeenea sana katika jamii za Afrika Mashariki.

Vile vile, dhima ya kutambulisha katika utani wa jamii ya Kiuyu Minungwini na Kojani inajitokeza katika miktadha ya minada ya samaki. Katika minada hiyo, watu hutania na kuambiana maneno ambayo yanawafanya watambuliwe kuwa ni wa jamii moja ama zilizona historia moja na uhusiano wa karibu. Mfano ufuatao unatudhihirishia hilo kama ifuatavyo:

- Dalali: “Haya papa huyunoooo lakini wengine wanapapa wao nyumbani lakini kalalie papa kwako usije ukalalia hapa?”
- Wachuuzi: Hamsini, sitini.
- Dalali: “Kampe mkeo hizo. Usinambie mie kuwa hutini. Mwambie akupikiaye chakula **kwako...**”

Dondoo hili linatusaidia kujua kwamba wahusika ni watu wa karibu na waliozoeana. Picha hii inapatikana kutokana na matumizi ya lugha yenye kubeba dhihaka na kejeli na pengine hata matusi miongoni mwa wahusika. Uteuzi huu wa lugha unaojidhihirisha katika dondoo hili ni ishara inayotubainishia kuwa wahusika wamezoeana jambo ambalo linawafanya wakengeushe lugha rasmi na kutumia lugha

yenye matusi. Lugha kama hiyo inatumika katika miktadha ya kutafuta wachumba wa kufunga nao ndoa. Tazama mfano ufuatao:

**Wakiuyu** Minungwini: Kojani hii hapana mke wa kumuoa hawana sifa ya kuingia mjini kwetu.  
**Wakojani:** Hawana walijualo tukiwapeleka kwetu ni aibu tupu tutakoma kuwaokoa na **maisha ya chumvi waliyonayo.**

Athari hii ya utambulisho kama inavyojidhihirisha katika nyimbo teule za Khadija Kopa linalandana na mawazo ya Fairclough (1989) anavyosema maneno hubeba itikadi za jamii. Hivyo mifano hiyo ya utani inalenga kudokeza itikadi ya jamii kuhusu maisha ya kila siku. Itikadi hizo zinapelekea wahusika kutambulika. Kwa kutumia nadharria ya Mwitiko wa Msomaji inayompa fursa ya kuihakiki kazi ya fasihi kutokana na uoni wake na tajiriba alizonazo, mtafitiamepata ujasiri wa kusema kuwa matumizi ya utani wa jamii ya Kiuyu Minungwini na Kojani hutumika kama sehemu ya kujitambulisha. Wanaposema “Wapeni chakula wale hawajalapo hao. Wapate pumzi za kurudi kwao.” Ni utani ambao umezoeleka na pale mtu anaposema hivyo au kuambiwa hivyo hadhira hutambua kuwa hawa ni Wakojani na Wakiuyu Minungwini.

#### **4.4.6 Kukuza Umoja na Mshikamano**

Vile vile, uchambuzi wa data unaonesha umuhimu wa kuleta umoja na mshikamano miongoni mwa wanajamii. Kwa mfano, katika shughuli za kilimo hutumika utani ambao unalengo la kusaidia katika kuleta umoja na mshikamano. Katika muktadha huo wa kilimo wanajamii huwasaidia wengine katika shughuli za kilimo na wanapokutana naye humtania kwa kumwambia:

“Ah! umvivu. Tunkufanyia hivyo ili uone watu wanavyoweza kufanya kazi kwa mara moja na sio kugongagonga.”



Katika dondoo hilo tunaona namna jamii inavyotumia utani ili kujenga umoja na mshikamano. Huu ni utani ambao una matokeo chanya kutokana na wahusika kupata fursa ya kuendeleza uzalishaji mali huku wakisaidiana. Hili linatupatia picha ya maisha ya vijijini ambapo wanawake wengi wamekuwa wakishiriki katika shughuli za kilimo kwa kusaidiana. Mhusika anapoambiwa kuwa “*Ah! Umvivu*” anaona kuwa ni sehemu ya utani hivyo kamwe hapaswi kuchukua bali mara nyingi huamua kuambatana pamoja ili kukamilisha kazi inayohusika.

Aidha, kundi la watani wanapomwambia yule aliyetaniwa na kusaidiwa katika kazi ya shambani kuwa “*tunachukua huu ndio malipo yetu*” anaridhika na hilo kwa sababu iwapo atakataa ama wale waliofanya kazi hiyo wamekataa kuchukua chochote inaonekana kuwa uhusiano uliopo sio mzuri miongoni mwa wahusika. Vile vile, katika miktadha ya msibani kuna utani ambao unaonesha namna jamii hiyo inavyotumia utani kama sehemu ya kuleta mshikamano miongoni mwa wanajamii.

Hili linadhahirika kutokana na dondoo lifuatalo:

Mtani: Asha ncho unigaile wanja na poda yangu na kile kioo kchangu.... Naona thiviyoni.

Asha: Ha, hivyo apo (anaikiwa poda, kioo, wanja na mtani anaanza kujiremba mbele ya hadhira mara anajigeuza huku mara anajitia wanja na mafuta-vicheko **vinasikika**).

Katika dondoo la hapo juu, tunajifunza kuwa wanajamii hufanya utani katika muktadha wa msibani ili kuwaliwaza wafiwa pamoja na kuonesha umoja katika tukio hilo la msiba. Nadharia ya Mwitiko wa Msomaji imesawiri suala la umoja na mshikamano miongoni mwa wanajamii. Kwa mfano, huko katika kisiwa cha Kojani ni jadi ya jamii hiyo kufanya utani pale anapofariki mtu wa makamo. Vile vile, shughuli kama vile za kilimo huchapuzwa kwa kutumia fani ya utani ndani yake.

Aidha, hata pale watani wanapowaambia wengine “*Wapeni chakula wale hawajalapo hao. Wapate pumzi za kurudi kwao.*” Wanalengo la kuonesha umoja na mshikamano na wala si udhalilishaji.

#### **4.4.7 Kuhimiza Kazi na Kuweka Akiba**

Kufanya kazi ni miongoni mwa mambo muhimu katika jamii, taasisi, taifa, mataifa pamoja na ulimwenguni kote. Bila ya kufanya kazi hakuna maisha wala maendeleo yoyote kwa jamii yoyote. Haya ni miongoni mwa maadili muhimu anayotakiwa kila mwanajamii kuyaelewa (Hassan, 2017). Data zilizokusanywa na mtafiti zimebaini kuwa utani wa jamii ya Kojani na Kiuyu Minungwini umekuwa ukihimiza kufanya kazi na kujiweka akiba kama inavyodhihirika katika dondoo lifuatalo:

**Mvuvi wa Kojani:** (Anamwambia baba yake wakiwa baharini)  
Hooo! Kazana huko. Jikaze samaki wasiaweee.  
We ukhanisi. Jikazeeee bwege.

Mvuvi Kiuyu: Jaaa! Wamwambia hivyo, yule mbabayo vyooo!  
Wamtukana huna akili!

Mvuvi wa Kojani: Enyondokeya hapawe. Wee bwege wa Kiuyu,  
miye si mtukani yeye naitukana kazi.

Katika dondoo hili tunaona namna kazi ya uvuvi inavyohamasishwa na mtoto dhidi ya baba yake. Kutokana na dondoo hili tunajifunza kwamba kila mwanajamii anatakiwa kufanya kazi ili kujenga jamii mpya endelevu. Pia, ipo haja ya kila mmoja kumuhimiza mwingine kufanya kazi. Kwa sababu ya umuhimu huo Mheshimiwa Rais wa awamu ya tano wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania alikuja na kauli mbiu ya “Hapa Kazi tu.” Aidha, katika kuhakikisha tunajenga jamii endelevu utani wa jamii ya Kojani na Kiuyu Minungwini unadhima ya kuhimiza kujieka akiba. Tazama mfano ufuatao namna unavyoisawiri dhima hiyo:

Mtani: Bibie niletee muhogo na samaki wote leo hakuna kubakisha kesho. Maana nyie **kila siku wasikia nataka**

**saza ngau cha kesho. Hapana kesho hapa. Kesho aijuaye ni Mlijuu. Kwani husikili kwamba kitoe ni kitoeo. Maanaye kiliwe leyo leyo...”**

Dondoo hilo ni mfano wa utani unaofanywa katika muktadha wa mazishi. Lengo la utani huu ni kuhamasisha kuweka akiba kwa ajili ya matumizi ya baadae. Kwa hivyo, tabia aliokuwa nayo marehemu inakosolewa kutokana na kutokubali kuweka akiba. Tunaporejelea nadharia ya Mwitiko wa Msoamaji mtafiti anakubaliana na mawazo yanayohimiza kazi na kujiekea akiba kutokana na ukweli kwamba bila kazi msingi wa maisha hudorora tangu ngazi ya mtu mmoja mmoja, familia na taifa kwa ujumla. Aidha, kile kinachopatikana ipo haja ya kuweka akiba. Huo ndio msingi imara wa kujenga maisha ya kesho yake. Kwa sababu hiyo Waswahili husema “Akiba haiozi.”

#### **4.4.8 Kuikosoa Jamii**

Data zinaonesha kuwa utani una dhima ya kuikosoa jamii kutokana nabaadhi ya matendo ya wanajamii. Kutokana na dhima hii utani huwa ni njia ya kuirekebisha jamii katika nyanja mbali mbali za maisha. Hivyo basi, ipo mifano kadhaa ya utani ambayo hutumiwa na jamii ya Kojani na ile ya Kiuyu Minungwini kuikosoa jamii kama ifuatavyo:

Mtani: “Huwezi kukaa nae ungekuja tuita tukamchukua bila shaka humuwezi ndio maana akakukimbia na mwengine tukisikia tutamuelekeza huyo si muume rudi kwenu.”

Katika mfano huo wa utani, mwanamme anakosolewa kutokana na tabia yake ya kushindwa kuishi vema na mkewe na matokeo yake mwanamke huyo amamua kuondoka katika ndoa hiyo. Haya ni maelezo ya utani anayopewa mwanamme wa Kojani na Kiuyu Minungwini pale wanapogombana na wake zao. Pia, katika utani huo wanaonywa kuwa huenda wasipate tena mke kutokana na tabia zao.

Mfano mwingine wa utani ulio na dhima ya kukosoa katika jamii ya Kiuyu Minungwini na Kojani ni ule unaohusu mtu kumtania asiyekuwa mtani wake. Tazama mfano wa utani ambao kijana wa Kojani alijikuta akimtania baba yake wakati wa kazi ya uvuvi. Mfano huo unajitokeza hivi:

**Mvuvi** wa Kojani: (Anamwambia baba yake wakiwa baharini)  
 Hoo! Kazana huko. Jikaze samaki wasiawe.  
 We ukhanisi. Jikazeeee bwege.  
**Mvuvi** Kiuyu: Jaaa! Wamwambia hivyo, yule mbabayoyooo!  
 Wamtukana huna akili!  
**Mvuvi** wa Kojani: Enyondokeya hapawe. Wee bwege wa Kiuyu,  
 miye si mtukani yeye naitukana **kazi**.

Katika dondoo hilo tunamuona jinsi Mkojani anavyokosolewa na Mkiuyu Minungwini kutokana na kutoa maneno ya matusi kwa baba yake kwa kisingizio kuwa anaitukana kazi. Utani huu unadhima ya kukosoa vijana ambao wamekuwa wakifanya utani bila ya kuzingatia uhusiano wa wahusika, jambo ambalo ni muhimu sana katika fani ya utani. Kama anavyoshadidia Mulokozi (1989) kwamba utani huzingatia miktadha na uhusiano wa watani hao.

Vile vile, utani wa jamii ya Kojani na Kiuyu Minungwini una dhima za kuikosoa jamii kuhusu matendo yasiyokubalika. Kwa mfano, utani huo umekuwa ukiwakosoa wanajamii ambao wanatabia ya kufanya ngono holela. Tazama mfano wa utani unaojitokeza katika usemezano kati ya Mkojani na Mkiuyu Minungwini wakiwa katika harakati za kwenda kuvua samaki kama ifuatavyo:

**Mvuvi** wa Kojani: Naona huwezi kufanya kazi mpaka uende ukapige goti “Je nende kazini au nisende bibie.”  
 Unamnyenyekea mkeo kama sanamu la kanisani. Hapa hatuna tu.  
**Mvuvi** wa Kiuyu: Miye nachonga mahaba na namridhisha mke wangu si kama weye unayeridhisha vimada.

Kichwa kikubwa kama cha tembo lakini akili hakina.

Kwa ujumla, baada ya mtafiti kutalii mifano kadhaa ya utani amebaini kuwa utani ni kiungo muhimu katika kuirekebisha jamii. Utani huyaweka wazi matendo yasiyofaa kama vile ya kufanya ngono holela, kushindwa kutunza ndoa nakadhalika. Kwa kutumia fani ya utani wanajamii hukosoa na kukosolewa bila ya kusababisha migogoro. Ingawa ili kulifanikisha hilo, inapasa mtu kuzingatia miktadha na uhusiano wa wahusika wakati wa kufanya utani.

#### **4.4.9 Kuendeleza Mila na Desturi za Jamii**

Mila na desturi ni sehemu ndogo ya utamaduni wa jamii. Vipengele vingine vya utamaduni ni silka, imani, itikadi na jadi za watu katika mazingira yao mahususi ya nchi yao, (Khamis 2016). Data zilizokusanywa na mtafiti zimeonesha kuwa utani wa jamii ya Kiuyu Minungwini na Kojani umekuwa ukisawiri mila na desturi za jamii hiyo kama ifuatavyo:

Katika jamii ya Kiuyu Minungwini ni desturi ya wanawake kuwatania Wakojani pale wanapotakiwa kuolewa na kwenda kuishi katika Kisiwa cha Kojani. Ili kuonesha hisia zao hujikuta wakieleza kama hivi:

“Sisi hatutaki kuondolewa mjini kwetu kwenye raha ya kila kitu na kupelekwa sehemu ambayo haina hata mchanga wa kusugulia masufuria na maji matamu ya kusugulia vyombo sisi tumezowea kuosha masufuria yetu yaseme na kiambaza na mtu akipita ajione alivyo...”

Katika dondoo hilo tunaona namna wanawake hao wanavyodai kuwa hawako tayari kuolewa na kuacha kuendelea na maisha katika kijiji chao ambacho kina kila aina ya maisha ya kuridhisha na kwenda kuishi Kojani ambako hakuna hata mchanga

unaotumika katika kuosha masufuria. Kwa ujumla mwitiko wa msomajiuligundua kwamba uzoefu wa maisha ya wanawake katika jamii ya Kiuyu Minungwini hawakatai kufunga ndoa na Wakojani, bali utani huu unatumika kama sehemu ya mila nadesturi ya wanawake hao.

Vile vile, utani wa jamii ya Kojani na Kiuyu Minungwini una dhima ya kuonesha mila na desturi za maisha ya jamii hizo. Katika utani huo tunaoneshwa namna jamii ya Kiuyu Minungwini ilivyo na ujuzi katika kupandia miti. Hili linaelezwa kupitia dondoo lifuatalo:

Mkiuyu Minungwini: Ni kiasi hawawezi kukwea miti kazi yao ni uvuvi tu waoneshe ujabari wao baharini na sio juu ya miti.

Utani huu hufanyika pale mkaazi wa Kojani kwa bahati mbaya anapopanda mti na kuanguka. Pamoja na kwamba kunakuwa ni sehemu ya ajali lakini utani huchukua nafasi yake kati ya jamii hizi ili kuonesha kuwa kitendo alichokifanya mhusika si desturi yake hivyo lilikuwa ni kosa. Kwa upande wa Wakojani, jamii ambayo ina uweledi katika kuogelea, anapozama mwanajamii kutoka Kiuyu Minungwini humtania kwa kusema:

Mkojani: Hiyo si kaziye. Haviji kuogelea na waliopo nyuma yake waache kazi ya baharini ina wenyewe wakojani la sivyo watasoza. Wacheza ngoma si yao. Hii ni kazi ya kiume.

Kwa ujumla mtafiti anaporejelea nadharia ya Mwitiko wa Msomaji amebaini kuwa utani wa jamii ya Kiuyu Minungwini na Kojani unasawiri mila na desturi za jamii hiyo. Kutokana na dhima hii utafiti umebainisha kuwa utani kama sehemu hutumika kuendeleza na kueleza mila na desturi za jamii husika kama mawazo haya yanavyoshadidiwa na Simiyu (2011) ambaye anaeleza kuwa kati ya majukumu ya

fasihi simulizi ni kueneza na kuhifadhi mila, desturi na amali za jamii kama vipengele vya utamaduni wa jamii.

#### **4.4.10 Kuburudisha**

Moja ya dhima muhimu kabisa ya kazi ya fasihi ni kuburudisha (Mulokozi, 1996). Data zilizokusanywa na mtafiti zinaonesha kuwa utani wa jamii ya Kiuyu Minungwini na Kojani umekuwa ukiiakisi dhima hii ya kuburudisha. Kutokana na dhima hii watu hujikuta wakifurahi na kucheka kutokana na utani huo. Kwa mfano, wakati wa misiba, wajukuu wanapotania katika kumuiga marehemu hadhira hujikuta ikifurahi na kucheka. Tazama mfano ufuatao:

Mtani: Asha ncho unigaile wanja na poda yangu na kile kioo kchangu.... Naona thiviyoni.

Asha: Ha, hivyo apo (anaikiwa poda, kioo, wanja na mtani anaanza kujiremba mbele ya hadhira mara anajigeuza huku mara anajitia wanja na mafuta-vicheko vinasikika)

Dondoo hilo ni mfano wa utani unaojitokeza wakati wa msiba. Lengo kuu la utani huo ni kuwaliwaza wafiwa na kuwafanya wacheke ingawa wamekabiliwa na msiba wa ndugu wa familia yao. Hili linashadidiwa katika utafiti wa Mgakanzila (2010) ambaye alifanya utafiti uliojikita kuchunguza suala la utendekaji katika utani wa Wasukuma. Katika utafiti huo Mgakanzila (keshatajwa) iligundulika kuwa utani wa Wasukuma una nafasi kubwa katika kufichua maovu ya jamii, furaha na viburudisho. Utani unaoibua furaha katika jamii ya Wasukuma hujitokeza kutokana na kuwaiga watu wanavyoangalia na wanavyotenda. Kutokana na ukweli huo, mtafiti akiongozwa na nadharia ya Mwitiko wa Msomaji anathibitisha kuwa utani wa jamii nyingi ukiwemo ule wa jamii ya Kojani na Kiuyu Minungwini unasadifu dhima hii ya kufurahisha.

#### **4.5 Hitimisho**

Katika sura hii mtafiti amefanya uwasilishaji na uchambuzi wa data za utafiti huu. Sura hii imepangiliwa kutegemea malengo ya utafiti huu. Kila lengo limefanyiwa uwasilishaji na uchambuzi wa data hadi pale majibu ya swali linalohusika na lengo la utafiti huo lilipokamilika. Wakati wa kufanya uchambuzi wa data nadharia ya Simiotiki na nadharia ya Mwitiko wa Msoamaji zilirejelewa hapa na pale kadri ilivyoonekana zimesadifu. Hivyo katika sura inayofuata utafiti umebainisha matokeo ya utafiti huu.



## **SURA YA TANO**

### **MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO**

#### **5.1 Utangulizi**

Sura hii inatoa muhtasari, hitimisho na mapendekezo ya utafiti huu. Kwenye sura hii ndio kunapatikana kwa muhtasari majibu ya maswali ya utafiti huu. Kimsingi sura hii inabainisha namna mtafiti alivyoyafikia malengo ya utafiti huu. Hivyo basi, sura hii imejibainisha kama ifuatavyo:

#### **5.2 Muhutitari wa Tasnifu**

Lengo kuu la utafiti huu lilikuwa ni Kuchunguza dhima za utani na namna fani hiyo inavyotumia lugha katika jamii ya watu wa Kiuyu Minungwini na Kojani. Ili kulifikia lengo hilo mtafiti aliongozwa na malengo mahususi matatu. Lengo mahususi la kwanza lilikuwa ni Kubainisha aina za utani wa jadi kati ya jamii za Kiuyu Minungwini na Kojani. Lengo hili liliongozwa na swali la utafiti lisemalo, ni aina zipi za utani wa jadi zinazojitokeza katika jamii za Kiuyu Minungwini na Kojani? Lengo mahususi la pili lilikuwa ni Kuchunguza vipengele vya lugha vinavyojitokeza katika utani wa jadi kati ya jamii ya Kiuyu Minungwini na Kojani. Lengo hili liliongozwa na swali la utafiti lisemalo ni vipengele vipi vya lugha vinavyojitokeza katika utani wa jadi kati ya wanajamii wa Kiuyu Minungwini na Kojani?. Na lengo mahususi la tatu lilikuwa ni Kuchambua dhima za utani wa jadi kwa jamii ya Kiuyu Minungwini na Kojani. Lengo hili liliongozwa na swali la utafiti lisemalo ni dhima zipi zinazojitokeza katika utani wa jadi wa wanajamii wa Kiuyu Minungwini na Kojani?

Tasnifu hii ina jumla ya sura tano. Sura ya Kwanza ni sura ya utangulizi ambayo inaeleza mambo ya msingi ya utafiti huu. Sura hii imebainisha na kueleza usuli wa mada ya utafiti, tatizo la utafiti, malengo ya utafiti, lengo kuu na malengo mahususi, maswali ya utafiti, umuhimu wa utafiti, mipaka ya utafiti na muundo wa tasnifu hii.

Sura ya pili inahusu mapitio ya kazi tangulizi na mkabala wa nadharia. Sura hii inasehemu yaistilahi muhimu zinazohusu sura hii, dhana ya utani na matumizi ya lugha katika fasihi. Aidha, sura hiyo inaeleza mapitio ya maandiko kuhusu utani. Mapitio hayo yamemuwezesha mtafiti kubainisha pengo la utafiti. Mwisho sura imeeleza nadharia ya Simiotikia na nadharia ya Mwitiko wa Msomaji ambazo zimeongoza utafiti huu.

Sura ya tatu ya tasnifu hii imeelezea mbinu za utafiti. Vipengele vilivyojumuishwa katika sura hii ni usanifu wa utafiti, eneo la utafiti na walengwa wa utafiti. Vipengele vingine vilivyooneshwa ni sampuli na mbinu za usampulishaji. Aidha, sura hii inaelezea aina za data na mchakato wa ukusanyaji wa data. Mwisho, sura inaeleza uthabiti na kuaminika kwa data na maadili ya utafiti.

Sura ya nne imefanya uwasilishajinauchambuzi wa data za utafiti huu. Sura hii imegawanyika katika sehemu ndogo ndogo tatu. Sehemu hizo zimepangwa kutegemeana na malengo ya utafiti huu. Sehemu ya kwanza imewasilisha na kuchambua data zihusuzo aina za utani wa jadi katika jamii ya Kiuyu Minungwini na Kojani. Sehemu ya pili ni uwasilishaji na uchambuzi wa data zinazohusu matumizi ya lugha katika utani wa jadi wa Kiuyu Minungwini na Kojani, na sehemu ya mwisho imebainisha dhima za utani wa jadi katika jamii ya Kiuyu Minungwini na Kojani. Uchambuzi wa data katika sura ya nne uliongozwa na nadharia mbili.

Nadharia ya Mwitiko wa Msomaji kwa upande mmoja na Nadharia ya Simiotiki kwa upande wa pili.

Sura ya tano imehitimisha kwa kutoa muhtasari wa utafiti, matokeo ya utafiti na mapendekezo. Sura hii inaeleza kwa muhtasari kile kilichogunduliwa na mtafiti. Maswali yaliyoongoza utafiti huu yanaelezwa majibu yake kwa ufupi kama ilivyobainika kupitia uwasilishaji na uchambuzi wa data katika sura ya nne ya tasnifu hii. Hivyo basi, matokeo ya utafiti huu yalikuwa kama ifuatavyo:

### **5.3 Muhutasari wa Matokeo ya Utafiti**

Utafiti huu ulikuwa na malengo mahususi matatu. Uchambuzi wa data umetoa matokeo kama ifuatavyo:

#### **5.3.1 Lengo Mahususi la Kwanza. Kubainisha aina za utani wa jadi katika jamii ya Kiuyu Minungwini na Kokjani.**

Lengo mahususi la kwanza la utafiti huu lilikuwa ni: Kubainisha aina za utani wa jadi katika jamii ya Kiuyu Minungwini na Kojani. Lengo hili liliongozwa na swali la utafiti la kwanza lisemalo: Ni aina zipi za utani wa jadi unaojitokeza katika jamii za Kiuyu Minungwini na Kojani?. Matokeo ya lengo hili, yalionesha kuwa utani wa jadi wa jamii ya Kiuyu Minungwini na Kojani unaweza kuwekwa katika utani wa misibani, utani wa shuguli za harusi, utani kwenye minada ya bidhaa, utani katika shughuli za uvuvi, utani unaohusu kujitambulisha, utani katika michezo, utani katika kuchumbia wachumba, utani wa matukio ya ajali na huzuni, utani katika vyombo vya usafiri na utani katika shughuli za kilimo.

### **5.3.2 Lengo Mahsusi la Pili Kuchunguza Vipengele vya Lugha Vinavyojitokeza katika Utani wa Jadi kati ya Wanajamii wa Kiuyu Minungwini na Kojani.**

Lengo mahsusi la pili la utafiti huu lilikuwa ni: Kuchunguza vipengele vya lugha vinavyojitokeza katika utani wa jadi kati ya wanajamii wa Kiuyu Minungwini na Kojani. Lengo hili liliongozwa na swali la utafiti lisemalo, ni vipengele vipi vya lugha vinavyojitokeza katika utani wa jadi kati ya wanajamii wa Kiuyu Minungwini na Kojani?. Matokeo katika lengo hili, yameonesha kuwa utani wa jadi katika jamii ya Kiuyu Minungwini na Kojani unatumia vipengele vya lugha ambavyo ni matumizi yalahaja, lugha ya kishairi, balagha, kejeli, dhihaka na lugha ya matusi.

### **5.3.3 Lengo Mahsusi la Tatu Kuchambua Dhima za Utani wa Jadi kwa Jamii ya Watu wa Kiuyu Minungwini na Kojani.**

Lengo mahsusi la tatu la utafiti huu lilikuwa ni: Kuchambua dhima za utani wa jadi kwa jamii ya watu wa Kiuyu Minungwini na Kojani. Lengo hili liliongozwa na swali la utafiti lisemalo Ni dhima zipi zinazojitokeza katika utani wa jadi wa wanajamii wa Kiuyu Minungwini na Kisiwa cha Kojani?Matokeo ya utafiti katika lengo hili yameonesha kuwa utani wa jadi wa jamii ya Kiuyu Minungwini na Kojani una dhima zakukuza lugha ya Kiswahili, kuendeleza utamaduni, kukuza fasihi ya Kiswahili, kutambulisha na kuifunza jamii. Dhima nyingine ni pamoja na kukuza umoja na mshikamano, kuhimiza kazi na kuweka hakiba, kuikosoa jamii, kuendeleza mila na desturi za jamii na kuburudisha.

## **5.4 Hitimisho**

Utafiti huu ulikuwa na lengo la kuchunguza dhima za utani wa jadi katika jamii ya Kiuyu Minungwini na Kojani. Utafiti umebaini kuwa utani wa jadi unaofanywa na

watu wa Kiuyu Minungwini na Kojani una dhima kubwa na kamwe hauwezi kubezwa. Dhima zake zina manufaa mbalimbali katika kuijenga na kuiendeleza jamii. Vipengele vya lugha vilivyotumika pia vinamchango wa aina yake katika kuiendeleza lugha ya Kiswahili.

## **5.5 Mapendekezo**

Utafiti huu unapendekeza kama ifuatavyo:

### **5.5.1 Mapendekezo kwa Watafiti Wengine**

Utafiti huu ulijikita kuchunguza dhima za utani wa jadi katika jamii ya Kiuyu Minungwini na Kojani. Hivyo ni wazi kwamba bado ipo nafasi ya kufanya tafiti nyengine katika utani wa jadihuku ukiwa na malengo tofauti na utafiti huu kama kuchunguza itikadi katika fani hiyo ya utani. Pia, tafiti zinaweza kufanyika kwa lengo la kuangalia namna majigambo ya jadi yanavyosawiriwa katika utani wa jamii zilizotafitiwa na jamii nyingine.

### **5.5.2 Mapendekezo kwa Jamii**

Utafiti huu unapendekeza kuwa wanajamii wakati wa kutumia utani ni vema kuepuka lugha iliyo na matusi. Pili, watani wanapaswa kuangalia uhusiano na miktadha ya utendaji wa utani ili kuepusha jamii kuingia katika mifarakano kutokana na matumizi ya utani. Mwisho, jamii inapaswa kuutumia utani kama nyenzo muhimu ya maisha kama kukuza na kuendeleza utamaduni wa jamii husika.

### MAREJELEO

- Adam, J. & Kamuzora, F. (2008). *Research Methods for Buisness and Social Studies*. Morogoro: Mzumbe Book Project.
- Ali, K. H. (2018). “Dhima ya Majina katika Vyombo vya Uvuvi kwa Jamii ya Watumbatu.” Tasnifu ya Uzamili MA-Kiswahili katika Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.
- Alhabib, E. (2012). “Matumizi ya Lugha katika Nyimbo za Taarab.” Tasnifu ya M.A Kiswahili Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.
- Enon, J.C. (1998). *Educational Research; Statistics and Measurement*. Kampala: Makerere University Press.
- Fadhili, F.E. (2014). “Kuchunguza Dhima ya Mtindo katika Tamthiliya za Historia: Utafiti Linganishi wa Tamthiliya za Morani na Kinjeketile.” Tasnifu ya Uzamli MA Kiswahili ya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.
- Faki, M.H. (2018). “Matumizi ya Lugha Tandawazi katiaka Mitandao ya Kijamii: Changamoto katika Lugha ya Kiswahili.” Tasnifu ya Uzamili MA-Kiswahili ya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.
- Gaichu, M.N. (2016). “Kuchunuza Sitiari Dhanfu Katika Methali za Kiswahili-Mtazamo wa Nadharia ya Uhusiano.” Tasnifu ya Uzamili ya MA-Kiswahili ya Chuo Kikuu cha Nairibi.
- Gaspar, I.C. (2012). *Methali, Nahau, Vitendawili na Mafumbo*. Dar es Salaam: Khashu Investment.

- Gichohi, F.G. (2018). "Utambulisho wa Wanaume katika Methali za Jamii ya Agikuyu." Tasnifu ya MA-Kiswahili ya Chuo Kikuu cha Egerton Njoro.
- Hassan, H.A. (2017). "Kuchunguza Fasihi ya Majina ya Mitaa Mjini Unguja." Tasnifu ya Uzamili MA-Kiswahili ya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.
- Jilala, H. (2016). *Misingi ya Fasihi Linganishi*. Dar es Salam: Daud Publishing Company.
- Julia, W. (2013). "Kanga kama Sajili Maalumu ya Kisanii na Mawasiliano." Tasnifu ya Uzamili MA-Kiswahili ya Chuo Kikuu cha Moi.
- Juma, A.R. (2015). Methali za Kswahili Zilizochwa: Sababu na Athai zake kwa Jamii. Tasnifu ya Uzamili MA-Kiswahili ya Chuo Kikuu cha Dodoma
- Kahmis, S. A. M. (1983). "Nafasi ya Fasihi Simulizi katika Jamii ya Tanzania." Katika Jarida la *Mulika Na. 15 uk. 3-13*.
- Khatib, T.O. (2017). "Dhamira Ziyengwazo na Taswira katika Methali za Wapemba." Tasnifu ya Uzamili MA-Kiswahili ya Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar.
- Kipacha, A. (2014). "Misemo katika Lugha za Magari: Divai Mpya?" Katika Jarida la *Swahili Forum Na. 21, uk. 104-121*.
- Kombo, D.K & Tromp, D. L. (2006). *Proposal and thesis Writing: An Introduction*. Nairobi: Paulines Publications Africa.

- Kothari, C.R. (2008). *Research Methodology: Methods and Techniques*. New Delhi: New Age. International Publishing Limited.
- Maitaria, J.N. (2012). "Uainishaji wa Ushairi wa Kiswahili kwa Kutumia Kigezo cha Methali." Katika *Mulika Na. 31, uk. 89-104*.
- Mahenge, P. (2009). "Semi zitumikazo kwenye Tiketi za Daladala," *MulikaNa 29 na 30*. Dar es Salaam: TATAKI.
- Massamba, M. (2004). *Kamusi ya Isimu na Falsafa ya Lugha*. Dar es Salaam: Tanzania Publishing House.
- Mbusya, C.M. (2019). "Mielekeo ya Wanafunzi wa Shule za Upili Kuhusu Methali Kinzani; Uchunguzi katika Kata ya Kitui Mjini; Kaunti ya Kitui." Tasnifu ya MA- Kiswahili ya Chuo Kikuu cha Southern Eastern Kenya.
- Migodela, W. (2017). "Dhamira za Maandishi ya Kuta za Vyooni Jijini Dar es Salam *Dhima ya Ushairi* katika Kuhifadhi Historia ya Lugha." Katika Jarida la *Mkwawa Journal of Education Na. 1 uk. 1-8*.
- Mmbaga, N.O. (1978). "Dhima ya Ushairi katika Kuhifadhi Historia ya Lugha." Katika Jarida la *Mulika Na. 14, uk. 19-26*.
- Mtesigwa, G.K. (2013). "Kuchunguza Matumizi ya Methali katika Jamii ya Wanyiramba." Tasnifu ya Uzamili MA-Kiswahili ya Chuo Kikuu cha Tanzania.



- Mulokozi, M.M. (1989). "Tanzu za Fasihi Simulizi." Katika Jarida la *Mulika Na. 21*, uk. 1-24. Mulokozi, M.M. (1996). *Fasihi ya Kiswahili*. Dar es Salaam: Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.
- Msuya, P.A. (1977). "Fasili ya Methali." Katika Jarida la *Mulika, Na. 9 uk. 29-31*.
- Nassor, H.J. (2016). "Semi Zilizoandikwa Kwenye Vyombo vya Safari vya Baharini Kisiwani Pemba." Tasnifu ya Uzamili MA-Kiswahili ya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.
- Ndungo, C.W. na Mwai, W. (1991). *Kiswahili Studies: Part Two*. Nairobi: University of Nairobi Press.
- Ndungo, C.M. & Waful, R.M. (1993). *Tanzu za Fasihi Simulizi*. Nairobi: University of Nairobi Press.
- Njogu, K. na Chimerah, R. (1999). *Ufundishaji wa Fasihi: Nadharia na Mbinu*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.
- Panneerselvam, R. (2012). *Research Methodology*. New Delh: PHI Learning Private Limited
- Sengo T.S.Y.M. (2009). *Sengo na Fasihi za Kinchi*. Dar es Salaam: AERA Kiswahili Research Products.
- Skuni, M.M. (2018). "Kuchunguza Jinsi Nahau za Kiswahili Sanifu Zinavyokwamisha Mawasiliano Fanisi kwa Wageni wa Lugha." Tasnifu ya Uzamili MA-Kiswahili ya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

- Sylvester, A.G. (2016). "Kuchunguza Dhima za Methali za Jamii ya Wasimbiti wa Rorya Mkoani Mara." Tasnifu ya MA-Kiswahili ya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.
- Taasisi ya Ukuzaji Mitaala (1988). *Kiswahili Sekondari*. Dar es Salaam: TUMI.
- Timothy, K.M. (2016). "Maana ya Usemi na Mazungumzo katika Mitandao ya Kijamii Hususan Facebook na Twetter." Tasnifu ya Uzamili MA-Kiswahili katika Chuo Kikuu cha Nairobi.
- Walliman, N. (2011). *Research Methods*: London: Routledge.
- Wafula, R.M. (1999). *Uhakiki wa Tamthiliya Historia na Maendeleo yake*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation
- Wafula, R.M. na Njogu, K. (2007). *Nadharia za Uhakiki wa Fasihi*. Nairobi: Jomokenyatta Foundation.
- Wamitila, K.W. (2002). *Misingi ya Nadharia ya Fasihi*. (Chapa ya Pli). Nairobi: Vide-Muwa Publications Ltd.
- Wamitila, K.W. (2010). *Kanzi ya Fasihi: Misingi ya Uchanganuzi wa Fasihi*. Nairobi: Vide-Muwa Publication Limited.
- Wamitila, K.W. (2013). *Kichocheo cha Fasihi Simulizi na Andishi*. Nairobi: Focus Publications Ltd.

## VIAMBATISHO

### *KIAMBATANISHO 1: MUONGOZO WA MASWALI YA USAILIKWA WATAFITIWA*

Mpendwa mhojiwa

Ninafanya utafiti kuhusu **Kuchunguza Dhima za Utani wa Jadi Kati ya Watu wa Kiuyu Minungwini na Kojani Wilaya ya Wete, Mkoa wa Kaskazini Pemba.**

Utafiti unalenga kubainisha matapo ya utani unaojitokeza katika jamii hizo, kubainisha matumizi ya lugha katika utani wa jadi kati ya jamii zinazotafitiwa, na kuchunguza dhima za utani wa jadi kati ya watu wa jamii ya Kiuyu Minungwini na Kojani. Nitashukuru sana ikiwa utajibu maswali haya kwa umakini, uwazi, usahihi na ushirikiano wa hali ya juu. Taarifa zote utakazozitoa zitakuwa ni siri baina yetu na hazitotumika kwa lengo jengine lolote zaidi ya lengo lililoelezwa hapo juu.

Maswali wenyewe ni kama yafuatayo:

Jaza taarifa hizi kwaumakini

Jina ..... Umri..... Jinsia.....

Anuani ya makaazi..... Nambari ya Simu.....

1. Unafahamu nini kuhusu utani?
2. Je, Wakojani na Wakiuyu Minungwini wana aina yoyote ya utani wa jadi?
3. Kama ndio nitajie angalau utani wa jadi wa aina tatu
4. Ni sababu zipi zinazowafanyawatu wa Kojani na Kiuyu Minungwini kutaniana?
5. Kuna dhima yoyote inayopatikana wakati utani unapotendeka?
6. Kama ndio nitajie angalau dhima tatu.

7. Je, unadhani utani wa jadi wa Kojani na Kiuyu Minungwini unaisaidia jamii hizi?
8. Kama ndio eleza kwa ufupi.
9. Ni makundi yapi hufanyiana utani zaidi?
10. Kama unayajua nitajie angalau mawili.
11. Kwa maoni yako, utani wa jadi unaofanyika katika jamii mbili hizi huipendeza jamii?
12. Kama ndio taja sababu mbili za msingi.

AHSANTE KWA USHIRIKIANO